BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,018,116,895/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Mfumo** wa utoaji mikopo elimu ya juu kufumuliwa

UKURASA 3



**Ronaldo ajibu kuhusu mustakabali wake Man Utd**

UKURASA 21


# Nipashe

Jumamosi Julai 30, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581022

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


# Serikali yatoa kauli nyongeza ya mishahara



**Yaweka** wazi utaratibu uliotumika katika upandishaji, yasisitiza milango iko wazi...

*Endelea ukurasa 2*



Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, akisaidiwa na mshtakiwa namba mbili, Sylivester Nyegu, kushuka kwenye gari la Magereza, baada ya kuwasili katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi, jana. Sabaya na wenzake wanne wanakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi . **PICHA: MARY MOSHA**

## Sabaya afikishwa mahakamani amefungwa bandeji kichwani

UK. 2

## Waziri atoa tahadhari kuibuka tena UVIKO - 19

UKURASA 3



MICHEZO **STARS KARATA MUHIMU LEO** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA), Adam Fimbo, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu mafanikio na utekelezaji wa shughuli za mamlaka hiyo, kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yatoa kauli nyongeza mishahara

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetoa msimamo kuhusu nyongeza ya mshahara kwa watumishi wa umma huku ikisema ililenga zaidi asilimia 75 hadi 78 ya watumishi wenye kipato cha chini.

Hivi karibuni, serikali imekuwa na majadiliano na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) kutokana na malalamiko ya nyongeza ya mshahara ambayo kima cha chini kimeongezwa kwa asilimia 23.3.

Akizungumza jana katika kikao kilichokutanisha serikali na viongozi wa wafanyakazi, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alisema kwenye upandishaji wa mishahara kuna utaratibu unatumika. Alisema wanapopandisha mishahara kima cha chini maana yake wanaangaliwa sana wale wafanyakazi wa kipato cha chini.

"Tukisema kima cha chini kinasaidia kupeleka mwelekeo hata kwenye sekta binafsi kwamba na huko mishahara kima cha chini kianzie hapo.

Sasa asilimia inayotamkwa inawalenga zaidi wale wenye kima cha chini si tu wale wanaoanza kazi bali hata waliotangulia kazi ambao wako kwenye kima cha chini kwa lengo la kuinua kiwango chao ili wapate fedha ambayo inaweza kukidhi mahitaji yao kutokana na mabadiliko ya uchumi nchini.

"Huku juu kwa watumishi wenye mapato makubwa hawapati ile asilimia kama inavyotamkwa tukiwalipa ile watakuwa wamekwenda mbali zaidi kuliko hawa wenye kipato cha chini kwa hiyo pengo la mishahara ndani ya serikali litakuwa kubwa," alisema.

Majaliwa alisema inatakiwa asilimia ipungue ili kuweka usawa wa mishahara na kuwaweka kwenye mfumo ambao hauweki pengo kubwa.

"Mnajua kupanda kwa mwisho tulipanda mwaka 2015 na kiwango cha upandaji wakati ule ilikuwa asilimia 13. Leo tumekwenda asilimia 23 kutokana na mabadiliko ya kiuchumi. Kwa mazingira ya sasa, inaonekana bado hakikidhi.

"Nataka niwaambie hata kama haikidhi, dhamira ya serikali ya kuboresha maslahi ya watumishi ambayo Rais ameionesha tuna matumaini huko baadae kupitia vikao hivi tunavyofanya ikiwamo hiki cha leo tunaweza kufikia hatua nzuri," alisema.

Hata hivyo, alisema upandishaji huo unafanyika kwa kuangalia hali ya uchumi nchini ili kutokwamisha kufanyika mambo mengine.

"Tunaangalia gurudumu hili la maendeleo tunaliendeshaje tusije kukimbiza ikafika mahali likatukwamisha, sisi sote ni watumishi wa umma au sekta binafsi kwa hiyo ni jambo letu," alisema.

Alibainisha kuwa lengo la kuwalenga wafanyakazi wenye kima cha chini ndilo kundi kubwa ambalo limenufaika na asilimia 23.3 na imekwenda hadi asilimia 20.

"Hawa wanaosema tumeongezwa Sh.20,000 ni wenye mishahara mikubwa wapo kwenye hii asilimia 22, humo ndimo unawakuta mawaziri, makatibu wakuu, wakuu wa mikoa, makatibu tawala wa mikoa, wakurugenzi na mameneja wa mashirika ambao na wao kidogo wana mshahara unaotosha.

"Ni asilimia 22 tu katika hili viongozi wenzangu wa wafanyakazi hawa ndio wamemudu hili jambo mpaka inaonekana ni shida ni tatizo lakini waliolengwa hii asilimia 23 hadi kushuka 20 ni asilimia 75."

"Huu ni utafiti ambao katibu mkuu wetu wa utumishi ameufanya baada ya kupitia madaraja na vile viwango. Lakini si wote wamepata asilimia 23 lakini wapo juu ya asilimia 20 kwa sababu ya ile tofauti.

"Ukiangalia kwa mfano mshahara wa waziri amepata 0.7, na amepata kwa sababu anakipato kikubwa na nyongeza yake ni ile ambayo imetamkwa huko," alisema.

"Ujumbe wa muhimu hapa ni kwamba asilimia 23 iliyotamkwa haijalipa watu wote ni kutokana na utaratibu unaotumika wa viwango vya mishahara na inapotamkwa wanaonufaika si wote mpaka wa mishahara mikubwa.

"Walionufaika ni wale wa kada ya chini ambao kwa tangazo la mwaka huu wanaonufaika ni hao asilimia 75 hadi 78."

"Sisi tuseme watumishi wetu wawaamini viongozi wa shirikisho la vyama vya wafanyakazi kwa sababu hata maslahi yaliyopatikana kipindi kilichopita zilikuwa jitihada zao, niseme hatuna ukomo wa kupokea lolote unaloliona kutoka vyama vya wafanyakazi nchini."

"Tutaendelea kutoa ushirikiano kwa vyama vyote niwahakikishie serikali ipo pamoja na nyie tutaendelea kupokea maoni na mapendekezo yenu ya namna bora ya kumfanya mfanyakazi afanye kazi ya kutoa matokeo chanya katika kuhudumia wananchi kwenye mambo mbalimbali," alisisitiza.

Awali, alisema Rais Samia Suluhu Hassan alisisitiza waambiwe ukweli na kwamba wanahitaji kupata muda zaidi wa kufanya maboresho makubwa.

"Rais (wa TUCTA,Tumaini Nyamhokya) ujio wenu hapa serikali imewaheshimu, tunatambua na tunathamini na kikao hiki kinalenga kuweka vizuri kwenye haya ambayo wafanyakazi wenzetu wanayasemea," alisema.

Majaliwa alisema Rais Samia tangu ameingia madarakani amekuwa akiboresha masuala ya wafanyakazi ikiwamo kulipa madai mbalimbali.

"Mwaka huu ameona ni wakati mzuri wa kuanza kupandisha mishahara ili kupata uzoefu wa kupandisha mishahara na maboresho yaliyofanywa nyuma yanalenga upandishaji wa mishahara,"alisema.

Julai 26, mwaka huu, Serikali na TUCTA walikutana kwa ajili ya kujadili suala hilo la mshahara uliolipwa Mwezi Julai mwaka huu ambalo wafanyakazi walionesha kutoridhishwa nalo.

Miongoni mwa hoja zilizowasilishwa na TUCTA kwa serikali alizowaambia waandishi wa habari, Rais wa TUCTA, Nyamhokya , alisema kiwango cha kima cha juu cha mshahara kisipungue asilimia 15.

Aidha, baadhi ya kada na taasisi za umma ambazo hazijaguswa na nyongeza hiyo ziangaliwe.

# Sabaya atinga kortini na bandeji kichwani

**Na Mary Mosha,** MOSHI

ALIYEKUWA Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, jana alifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Moshi akiwa amevikwa bandeji kichwani.

Taarifa za ndani zilidai kuwa Sabaya ambaye pamoja na wenzake wanne wanakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi, alifanyiwa upasuaji wa uvimbe uliokuwa umeta kisogoni, mapema wiki hii.

Ingawa haikuelezwa wazi mahakamani hapo amefanyiwa katika hospitali gani, Sabaya mwenyewe alidai nje ya mahakama kuwa alifanyikwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC mjini hapa.

Mbali na Sabaya, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Sylivester Nyegu, John Aweyo, Nathan Msuya na Antoro Assey.

Wakati kesi hiyo ilipotajwa jana, Wakili wa Utetezi, Helena Mahuna, akishirikiana na Fridolin Bwemelo, alimweleza Hakimu Mkazi Elibariki Phillii kuwa licha ya mteja wake kufika mahakamani, ni mgonjwa kutokana na kufanyiwa upasuaji wa uvimbe kwenye kisogo chake ambao aliupata akiwa mtumishi wa umma.

Alidai kuwa hali ya mshtakiwa huyo namba moja ni mbaya na inazidi kuzorota huku akidai kuwa iwapo kesi hiyo itaendelea kutajwa, inaweza kuathiri siku ya usikilizwaji kwa kuwa hali inaweza kuwa mbaya zaidi.

"Mheshimiwa hakimu, bado tunaiomba mahakama yako tukufu iuelekeze upande wa Jamhuri kukamilisha upelelezi pamoja na kibali kutoka ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP),ili kusikiliza kesi hii. Mshtakiwa ni mgonjwa akizidiwa hapa kesi itakuwa ngumu kusikilizwa.

"Tunaomba upande wa Jamhuri utuambie bayana ni nini kinaendelea. ikumbukwe mara ya kwanza kesi hii ilipofikishwa mbele ya mahakama yako, tulielezwa upelelezi umekamilika na waliomba tarehe ya karibu ili kesi ianze kusikilizwa lakini wameendelea kutupiga kalenda kwa mara

ya sita sasa. Mshtakiwa wa kwanza ni mgonjwa na afya yake inazidi kuzorota," alidai Mahuna.

"Washtakiwa wanazidi kuteseka hasa mshtakiwa namba moja ambaye hali yake ni mbaya. Kesi inaendelea kutajwa tu, hata haijaanza kusikilizwa. Tunaomba upande wa Jamhuri ukamilishe taratibu zinazohusika au waseme kama wameanzisha upelelezi mwingine ili tujue," aliongeza.

Naye Wakili Bwemelo alidai kuwa mshtakiwa namba moja amefanyiwa upasuaji mkubwa wa kichwa, hivyo anatakiwa apate huduma muhimu pamoja na uangalizi wa karibu na kuongeza kudai kuwa uvimbe huo ulitokea akiwa kazini.

"Ikiwa upelelezi haujakamilika na hawana taarifa za kutosha basi washtakiwa waachiwe huru. Jamhuri ikamilishe kila kitu ikiwa ni pamoja na kukamilisha upelelezi ili kesi ianze kusikilizwa," alidai Bwemelo.

Katika maombi yake ya msingi, Wakili wa Jamhuri, Sabitina Mcharo, aliomba mahakama kupanga tarehe nyingine kutokana na kutokamilika kwa upelelezi licha ya kwamba bado hawajapata kibali kutoka kwa DPP cha kuipa mahakama hiyo hadhi ya kusilikiliza kesi hiyo.

Baada ya hoja hizo, Hakimu Philli aliuhoji upande wa Jamhuri kutaka kujua kama upelelezi umekamilika ingawa kilichobaki ni kibali au la.

Wakili wa Jamhuri alijibu kwamba upelelezi haujakamilika pamoja na upatikanaji wa kibali kutoka kwa DPP. Kutokana na majibu hayo, Hakimu aliahirisha kesi hiyo hadi August 12, mwaka huu na washtakiwa wataendelea kukaa rumande kutokana na kesi hiyo kutokuwa na dhamana.

# Waziri atoa tahadhari kuwapo UVIKO-19

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imetoa tahadhari dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19 kuwa upo na kuwataka wananchi kuzingatia kanuni zote za kukabiliana nao ikiwa ni pamoja na uvaaji wa barakoa.

Aidha, waganga wakuu wa mikoa wametakiwa kuhakikisha katika sehemu zote za umma, kunakuwa na vifaa vya kunawia, maji tiririka pamoja na sabuni au vitakasa mikono.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alitoa tadhahari hiyo na agizo hilo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumzia kuhusu tahadhari ya UVIKO-19 na ugonjwa wa Mgunda ambao uligundulika Julai 18, mwaka huu mkoani Lindi kwa watu 20 na watatu kati yao kufariki dunia.

Ummy alisema ugonjwa wa UVIKO-19 bado upo nchini na kuwataka wananchi kuzingatia kanuni mbalimbali za kujikinga.

"Tujikinge na ugonjwa huu ikiwamo kuvaa barakoa hasa tukiwa ndani kama hapa tulitakiwa kuvaa barakoa kwa sababu wengi hamjachanja, tuhakikishe tunanawa mikono mara kwa mara.

"Ninarudia tena kuwataka waganga wakuu wa mikoa kuhakikisha sehemu zote za umma kunakuwa na vifaa vya kunawia mikono, maji tiririka pamoja na sabuni au vitakasa mikono. Tunataka vifaa hivyo virudi tena katika ofisi zetu kwa ajili ya kujikinga na magonjwa ya kuambukiza ukiwemo ugonjwa wa kipindupindu na kuhara damu," alisema. Waziri huyo alisisitiza wananchi waendelee kujitokeza kuchanja kwa sababu mwamko unaonekana ni mzuri.

"Endapo tutafikia asilimia 50 ya watu wenye umri wa miaka 18 na kuendelea wamechanja, maana yake tutakuwa tunakaribia kujenga kinga ya jamii. Takwimu zinaonyesha hadi jana (juzi) watu milioni 13.4 sawa na asilimia 43 ya Watanzania wenye umri zaidi ya miaka 18 na kuendelea," alisema.

Ummy alisema asilimia 99 ya watu wote inapotokea ameugua ugonjwa huo na kulazwa ni wale ambao hawajachanja. Kuhusu ugonjwa wa homa ya mgunda, Waziri Ummy alisema serikali inafunga rasmi kutoa taarifa zake na kuwataka wataalam waendelee kuelimisha umma dhidi ya magonjwa mbalimbali.

Alisema tangu wapokee taarifa rasmi za ugonjwa huo, hakuna mgonjwa mpya na idadi ya wagonjwa waliothibitishwa kimaabara kuugua walikuwa ni 20 na vifo vilikuwa vitatu kama vilivyoripotiwa awali.

Kwa mujibu wa Ummy, hadi sasa hakuna mgonjwa yeyote ambaye amelazwa katika kituo cha afya na kwamba umeonyesha unatibika kwa kutumia dawa zinazopatikana hospitalini.

"Timu ya ufuatiliaji imebaini miongoni mwa watu waliotangamana na wagonjwa ambao ni 15 wote wamepimwa na wameonekana hawana dalili wala maambukizi hadi sasa. Hii inadhihirisha pia ni mara chache ugonjwa huu kuambukizwa kutoka kwa binadamu mmoja kwenda mwingine," alisema. Alisema wataalam wanaendelea na utafiti wa kina kwa binadamu, wanyama na mazingira yanayowazunguka ili kubaini na kuweka mikakati ya kudhibiti ugonjwa huo nchini. Pia aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari zote za kujikinga hususan kuepuka kutumia maji au vitu vilivyochafuliwa na mkojo wa wanyama na kunywa maji safi na salama.

"Wagonjwa wenye dalili za homa, kuvuja damu, kichwa kuuma na mwili kuchoka wahakikishe wanafika kwenye vituo vya afya mapema ili wapate uchunguzi na matibabu sahihi," alisisitiza.

Sambamba na hilo, alisema wizara inawasisitiza wananchi kutoa taarifa za wagonjwa wanaoonyesha dalili tajwa.

Kadhalika aliwataka watoa huduma nchini kutoa taarifa kwa wakati kwa wizara kupitia mfumo wa ufuatiliaji magonjwa na waganga wakuu wa mikoa na wilaya kuimarisha na kufufua timu za ufuatiliaji wa magonjwa na kuzifuatilia tetesi zozote zinapojitokeza.




Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mwelekeo wa wizara, vipaumbele na maeneo ya kimkakati katika utekelezaji kwa mwaka wa fedha wa 2022/23. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mfumo mikopo elimu ya juu kufumuliwa

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imeunda timu maalumu ya kupitia mfumo wa utoaji wa mikopo ya elimu ya juu ili kuhakikisha kila mwanafunzi mwenye sifa anapata huduma hiyo.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema hayo jana Dar es Salaam wakati akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari.

Alisema lengo la kufanya mapitio hayo ni kuhakikisha mikopo hiyo inatolewa kwa wanafunzi wote wenye sifa na kuondoa urasimu.

"Tumeona kuna kazi nzuri ambayo inafanywa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) lakini tunataka kuendelea kuboresha zaidi utoaji wa mikopo hiyo. Sasa kuna timu ya wataalamu ambayo imeundwa kupitia mfumo mzima wa utoaji wa mikopo hiyo," alisema Prof. Mkenda.

"Lengo ni kutaka kila mwanafunzi mwenye sifa ya kupata mkopo anayechaguliwa kujiunga na elimu ya juu apate. Hii ni haki ya kila mtu, hivyo tunataka angalau kufahamu kwa kipindi cha miaka mitano namna ambavyo mikopo imekuwa ikitolewa, je vile vigezo ambavyo vinafahamika na wananchi vinafuatwa?

"Kwa hiyo tunakaribisha watu watoe taarifa, kwa mfano kama una wasiwasi wowote kuhusiana na utoaji wa mikopo hiyo. Ni vyema uje kutoa taarifa au kama kuna mwanafunzi ulisoma naye na una taarifa zake unakaribishwa. Tunachotaka ni kuhakikisha mikopo inatolewa kwa haki.

"Tunataka kufahamu pia kama kuna 'room' (nafasi) ya watu kupiga simu na kusema mwanangu yuko hapo mpe mkopo. Kama kuna nguvu ya watu wenye ushawishi wa kutaka watoto wao wapate mikopo wakati wao wana uwezo wa kulipa pia tujue," alisema.

Prof. Mkenda pia alisema Rais Samia Suluhu Hassan ametoa ufadhili wa masomo wa Sh. bilioni tatu kwa mwaka huu kwa wanafunzi ambao wamefanya vizuri katika masomo ya sayansi, uhandisi na elimu tiba kwenye vyuo vikuu.

Akizungumzia kuhusu maboresho yanayofanywa katika sekta ya elimu katika eneo la sera, mitaala na sheria, Prof.Mkenda alisema mchakato wa kukamilisha maboresho hayo unahitaji muda wa kutosha ili kuhakikisha kwamba maboresho hayo hayatakuwa ya kukurupuka.

"Mwaka huu bado tunaendelea kupokea maoni ya namna ya kuboresha sera, mitaala na sheria zetu na baada ya hapo, mchakato wa uamuzi utakuwa unatolewa kwa awamu, kikubwa zaidi tunachokwepa hapa ni kukurupuka. Hatutaki kufanya maboresho ambayo tukikaa kidogo yahitaji maboresho mengine tena," alisema Prof. Mkenda.

Kazi hii ya kuboresha sekta ya elimu ni mpango ambao umeanzishwa na serikali si wa Waziri. Kwa hiyo ni jambo ambalo ni lazima litakamilishwa," alisisitiza.

Alisema wizara hiyo bado inakaribisha wadau na makundi mbalimbali kutoa maoni yao katika kufanikisha maboresho hayo kwenye sekta ya elimu nchini.

## Ripoti ya shisha yatua kwa waziri

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RIPOTI ya uchunguzi wa bidhaa zinazochanganywa kwenye shisha uliofanywa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA), imekamilika na tayari imekabidhiwa kwa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu. Mei, mwaka huu, Waziri Ummy aliagiza TMDA kufanya tathmini hiyo ndani ya miezi miwili kutokana na kudaiwa shisha inachanganywa na baadhi ya bidhaa zinazosemekana ni dawa za kulevya.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Adam Fimbo, alisema: "Wakati wa Siku ya Kutovuta Tumbaku, Waziri aliagiza tufanye tathmini. Sasa imekamilika tumemkabidhi Waziri ndiye atakayetolea taarifa kwa sababu yeye alituelekeza tumefanya na tumemkabidhi." Aidha, Fimbo alisema mamlaka imeweka mfumo wa udhibiti wa bidhaa za tumbaku hadi sasa wameshatambua bidhaa zote za tumbaku zilizopo kwenye soko ambapo idadi yake hadi sasa ni bidhaa 51. "Mamlaka imeanzisha maabara ya upimaji wa bidhaa za tumbaku kwenye jengo lake lipo Dodoma,"alisema.

Kuhusu mafanikio ya taasisi kwa mwaka 2021/22 na matarajio ya mwaka 2022/23, alisema mamlaka imefanya operesheni tatu maalum kwenye Mikoa 14 na kukamata dawa bandia aina nne, dawa duni aina tano ,dawa za serikali na zisizosajiliwa.

Alisema dawa, vifaa tiba na vitendanishi vilivyokamatwa kwa kutosajiliwa vilikuwa na thamani ya Sh.milioni 353 na hatua zimechukuliwa dhidi ya watuhumiwa.

Hata hivyo, alisema kiasi cha bidhaa duni na bandia katika soko kimekuwa kikipungua ambapo hadi sasa tatizo la dawa duni na bandia lipo asilimia moja.

Kuhusu uteketezaji wa bidhaa zisizofaa kwa matumizi, Fimbo alisema bidhaa za dawa na vifaa tiba visivyofaa kwa matumizi ya binadamu zilizoteketezwa zimeongezeka kutoka tani 14,704.8 zenye thamani ya Sh.Bilioni 8.5 kwa mwaka 2022/21 na kufikia tani 35,547.4 zenye thamani ya Sh.bilioni 35.53 kwa mwaka 2021/22. "Kuongezeka kwa bidhaa zilizoteketezwa ni kutokana na kuimarisha ukaguzi na elimu kwa umma inayosaidia wateja kutoa taarifa juu ya bidhaa zisizofaa kwa matumizi," alisema.

Akizungumzia uchunguzi sampuli za bidhaa, Fimbo alisema wamechunguza sampuli 1,808 kwa mwaka 2021/22 ambapo kati ya hizo 1,644 sawa na asilimia 91 zilifaulu. Kadhalika, alibainisha mipango ya mwaka 2022/23, ni kuimarisha ukaguzi wa bidhaa kwenye vituo vya forodha na maeneo ya biashara za dawa, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa za tumbaku.

"Kukamilisha ujenzi wa miradi ya matanuri ya kuteketeza bidhaa zisizofaa yatakayojengwa mikoa ya Pwani na Dodoma,"alisema.

# Waziri abainisha vipaumbele vitano mwaka 2022/23

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

OFISI ya Waziri Mkuu, imetangaza vipaumbele vitano katika bajeti yake ya mwaka 2022/23 ikiwemo kuwasilisha bungeni muswada wa sheria mpya ya maafa ya mwaka 2021, inayolenga kujenga uwezo wa vyombo vya dola kukabiliana na majanga.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu vipaumbele vya bajeti ya ofisi hiyo.

Simbachawene alisema sheria hiyo itasaidia kuboresha mifumo ya usimamizi wa menejimenti ya maafa ya mwaka 2004 kwa ajili ya kuboresha mfumo wa uratibu na usimamizi wa maafa nchini. "Pia kipaumbele kingine ni kuendelea kujenga uwezo wa kuzuia, kujiandaa na kukabili maafa kwa kamati za maafa katika ngazi za mikoa, halmashauri, serikali za mitaa na wadau wengine na kukamilisha ujenzi na kuanzisha kituo cha kupokea taarifa mbalimbali za maafa eneo la Nzuguni 'B', jijini Dodoma" alisema Simbachawene.

Hata hivyo, alisema wataendelea kujenga uwezo wa kuzuia, kujiandaa na kukabili maafa kwa kamati za maafa za ngazi za mikoa, halmashauri na serikali za mitaa pamoja na wadau wengine.

Kuhusu mapambano dhidi ya biashara ya dawa za kulevya, alisema katika mwaka wa fedha wa 2022/23, Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya imeidhinishiwa Sh. bilioni 11.9 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake.

Alisema ongezeko la bajeti hiyo litaendelea kuimarisha udhibiti wa biashara na matumizi ya dawa za kulevya nchini. "Katika mapambano dhidi ya Ukimwi, Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania imeidhinishiwa Sh. bilioni 14.9 na kati ya hizo, Sh. bilioni 2.9 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ilihali Sh. bilioni 12 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ukilinganisha na bajeti ya Sh. bilioni 4.3 iliyotengwa mwaka 2021/22 ambapo ni sawa na ongezeko la asilimia 71.2," alisema.

Kadhalika, alisema shughuli zitakazotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2022/23 ni pamoja na kuratibu upatikanaji wa huduma za Virusi vya Ukimwi (VVU) na Ukimwi kwenye mikoa ya kipaumbele ikiwamo Iringa, Kagera, Katavi, Mbeya, Mwanza, Njombe, Pwani, Ruvuma, Shinyanga, Dodoma, Geita, Tabora na Songwe kwa ajili ya kuweka kipaumbele katika kuzuia maambukizi ya VVU kwa vijana wa miaka 15 hadi 24.

Kuhusu kukuza demokrasia nchini, alisema serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali na hivi sasa iko katika hatua ya kukamilisha ujenzi wa jengo la makao makuu ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya siasa jijini Dodoma.

Alisema ili kutekeleza shughuli hizo, serikali imeitengea Sh. bilioni 21.9 ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ili kutekeleza majukumu yake na kuongeza kuwa imeitengea Tume ya Taifa ya Uchaguzi Sh. bilioni 10, kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake.



Balozi wa Jamhuri ya Saharawi hapa nchini, Mahayub Buyema Mahafud (C), akipata maelezo kwa Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe, alipotembelea chumba cha habari cha kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Mikocheni Viwandani, mkoani Dar es Salaam jana. Kushoto ni Meneja wa Fedha wa TGL, Samuel Orgeness. **PICHA: JOHN BADI**

# Shaka asema Kinana chuo kikuu cha siasa

**Na Mwandishi Wetu,**

MBEYA

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, amesema Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, Kanali Mstaafu Abdulrahman Kinana, ni sawa na chuo kikuu cha siasa kinachotembea.

Shaka amesema hiyo ni kutokana na uwezo, weledi na ukongwe katika siasa za ndani na nje ya nchi.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza katika mkutano wa ndani uliohusisha wanachama wa CCM mkoani hapa ambapo ametumia nafasi hiyo kuelezea uwezo wa Kinana katika medani ya siasa.

"Leo (jana) nina utambulisho maalumu kwa wana Mbeya ukilinganisha na huko ambako tumepita. Tulianza ziara tarehe 25 kwa kuanza na Mkoa wa Katavi, tukaenda Rukwa, Songwe na leo tuko Mbeya.

"Nawashukuru sana. Kwanza namshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kumteua Kinana kuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara. Wajumbe wa Mkutano Mkuu nawashukuru kwa kumpitisha Kinana. Kabla sijafanya huo utambulisho, niwaambie kwamba amekulia ndani ya TANU na hatimaye CCM.

"Kinana ni gwiji la siasa za ndani na nje ya Tanzania. Kinana ni chuo kikuu cha siasa ambacho kinatembea. Wana CCM hasa vijana tuna kila sababu ya kujifunza kupitia yeye, tutembee katika nyazo zake," alisema.

Shaka baada ya kutoa maelezo hayo kuhusu uwezo wa Kinana katika medani ya siasa ametumia nafasi hiyo kuwatambulisha rasmi wana CCM Mkoa wa Mbeya kwamba Kinana ndio mlezi wa mkoa huo.

"Kinana ndiye mlezi wa CCM Mkoa wa Mbeya, uzuri wa chama chetu ulezi wetu sio wa kuchapana fimbo bali ni wa kushauriana na kupeana mawazo ya kujenga chama," alisema.

Katika hatua nyingine Shaka alisema kwamba kazi kubwa na nzuri ambayo inafanywa na Rais Samia katika kuwatumikia Watanzania wakiwemo wa mkoa wa Mbeya ni ukweli anaufuta upinzani.

"Kwa waliosoma shule wanajua kufuta kwa ufutio lakini Rais Samia anaufuta upinzani kwa kuleta maendeleo, hivyo kazi kwenu wana Mbeya ifikapo mwaka 2025," alisisitiza.

# Makamba: Umeme si kuwashaa taa pekee

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amesema serikali haisambazi umeme Vijijini kwa ajili ya kuwasha taa peke yake bali kuchagiza shughuli za kiuchumi ikiwamo uanzishaji wa viwanda.

Makamba aliyasema hayo juzi baada ya kutembelea kiwanda kinachochakata parachichi ili kutengeneza mafuta cha KUZA AFRIKA, Rungwe mkoani Mbeya ambacho kimeunganishiwa nishati hiyo na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Alisema uwapo wa kiwanda hicho ni matokeo ya uwekezaji mkubwa unaofanywa na serikali katika sekta ya nishati ambao umezaa matunda kwa kuwa kiwanda hicho pamoja na kuongeza thamani mazao ya wakulima, kimezalisha ajira zaidi ya 200 ndani ya kiwanda na katika mashamba ya parachichi.

Aliongeza kuwa msingi mzima wa kupeleka umeme Vijijini ni kusawazisha maendeleo kati ya watu wa Vijijini na Mijini kwa kuwa shughuli za kiuchumi kama za viwanda zinaboresha pia uchumi wa wananchi wa Vijijini.

Meneja wa TANESCO Wilaya ya Rungwe, Mhandisi Mukhsin Kijemkuu, alimweleza Waziri Makamba kuwa kiwanda hicho kabla ya kufungiwa transforma yake, kilikuwa kikizalisha lita 2,000 kwa siku lakini baada ya kupata transfoma wiki moja iliyopita, sasa kinazalisha lita 4,000 kwa siku.

Aliongeza kuwa kwa lita 4,000 zinazotarajiwa kuzalishwa kwenye kiwanda hicho mwekezaji angetumia Sh. milioni 50 kununua dizeli ya kuendesha mitambo lakini kwa sasa anatumia takriban Sh. milioni 30 kwa gharama za umeme.

Pamoja na kuishukuru wizara kwa kutenga fedha za kupeleka umeme kwenye maeneo kama hayo, Mhandisi Mukhsin aliwakaribisha wawekezaji wengine kwenye miradi kama hiyo kwa KUWA hali ya upatikanaji umeme sasa imeimarika na pia TANESCO itaongeza mapato yake.

Katika hatua nyingine, Waziri alifika kwenye Kijiji cha Iramba, wilayani Rungwe ili kukagua kazi zinazoendelea katika chanzo cha Jotoardhi cha Kiejo-Mbaka ambacho kinatarajiwa kuzalisha umeme utakaoingizwa kwenye gridi ya taifa.

Waziri Makamba baada ya kukagua chanzo hicho, alisema serikali imeamua kuweka nguvu katika kuzalisha umeme kwa njia mbalimbali.

"Tuna umeme wa maji, gesi, na safari hii tumewekeza kwenye umeme wa jotoardhi. Hapa Kiejo ni moja ya vyanzo vya jotoardhi ambavyo vina uwezekano wa kuzalisha umeme," alisema.

Alisema katika bajeti ya mwaka 2022/23, serikali imetenga Sh. Bilioni tano kwa ajili ya kuendeleza miradi hiyo na kwamba imenunua mtambo maalumu wa kuchoronga mpaka kilometa tatu chini ili kulifikia joto ambalo litatoa mvuke utakaozungusha mtambo wa kuzalisha umeme.

## HABARI KITAIFA



Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Kanali mstaafu Abdulrahman Kinana (kulia), akizungumza na wanachama na viongozi wa CCM na serikali wa mkoa wa Mbeya, jana. **PICHA: CCM**

# Vishikwambi sensa kunufaisha elimu

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema itasambaza shuleni vishikwambi ambavyo vitatumika katika sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti 23 mwaka huu.

Akizungumza na Wahariri wa vyombo vya habari jana, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Aldof Mkenda, alisema vishikwambi hivyo vitasambazwa shuleni baada ya kazi ya sensa kumalizika.

"Serikali imepanga kusambaza shuleni vishikwambi ambavyo vitatumika kwenye kazi ya sensa ya watu na makazi, hivi vitasambazwa baada ya kazi hii kumalizika," alisema Prof.Mkenda.

Alisema wanaamini kwamba kusambazwa kwa vishikwammbi hivyo kutasaidia kupunguza baadhi ya gharama ambazo zimekuwa zikitumika shuleni kufundishia.

"Kwa mfano kwenye eneo la karatasi, tunaamini kwamba baada ya kusambaza vishikwambi hivi vitasaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza baadhi ya gharama hususani matumizi ya karatasi.

"Na hili halitasumbua kwa sababu mkongo wa taifa umefika kote huko, kwa hiyo excess ya kuvitumia haitakuwa na shida," alisema.

Kwa mujibu wa Prof. Mkenda, kusambazwa kwa vishikwambi hivyo shuleni, kutasaidia kuongeza zaidi ufanisi wa ufundishaji na ujifunzaji shuleni.

Kazi ya sensa ya watu na makazi, inatarajiwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu, na itafanyika kidigitali na moja ya vifaa ambavyo zitatumika kukamilisha kazi hiyo ni vishikwambi.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa serikali, vishikwambi vinavyohitajika kwa nchi nzima kwa ajili ya kufanikisha kazi hiyo ni zaidi ya 200,000.

# TEC, vyama vya siasa vyajadili maazimio uchaguzi huru na haki

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KUTOKANA na uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan wa kuimarisha demokrasia ya vyama vingi nchini, Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) kwa kushirikiana na madhehebu mengine ya dini, limevikutanisha vyama mbalimbali vya siasa ili kutoka na maazimio yatakayosaidia uchaguzi mkuu kuwa huru na haki.

Katibu Mkuu wa TEC, Dk. Charles Kitima, aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye kongamano maalum la masuala ya demokrasia lililoandaliwa na baraza hilo kwa kushirikiana na taasisi ya Electoral Institute for Sustainable Democracy in Africa (EISA).

Alisema kongamano hilo lilikuwa likiangalia yaliyotokea kwenye uchaguzi mkuu uliopita na kuweka maazimio ya uchaguzi ujao ili kuwa huru na haki katika mchakato wake.

Kitima ambaye pia ni mratibu wa mafunzo hayo, alisema waliomba fedha kutoka Umoja wa Ulaya ili kukutanisha vyama vya siasa na wataalamu wabobezi kutoka nchi zilizopitia mikwamo hiyo zikiwamo Ghana, Malawi, Zambia na Afrika Kusini.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika, alisema viongozi wa dini kwa kushirikiana na vyama vya siasa wana mchango mkubwa katika kuendelea kuimarisha misingi ya demokrasia nchini.

Alisema kongamano hilo limewaweka pamoja na kwamba wamejifunza kuwa msingi mkuu wa demokrasia na tume huru ni Katiba.

"Ili kufikia malengo haya, ni vema watawala wakakubali kurudi kwenye mchakato wa katiba wakianzia na rasimu ya wananchi ambayo maoni yao yalikusanywa na iliyoitwa Tume ya Warioba," alisema.

Alisema kama kuwapo wa Katiba mpya hautafanikiwa ni vyema yafanyike marekebisho makubwa ili kuruhusu Tume huru ya uchaguzi ambayo itafuta maumivu yote.

"Yaliyopita nyuma hayakuwa mambo ya kufurahisha ambayo tusingependa yatokee tena, tangu Desemba mwaka 2019 tumedai meza ya mazungumzo hivyo penye mazungumzo ya haki kwa maslahi ya watanzania, hatasusia," alisema.

Naye Kiongozi Mkuu wa ACT Wazalendo, Zitto Kabwe, alisema kilio cha uwapo wa tume huru ya uchaguzi kimekuwa cha muda mrefu lakini sasa wanaamini kuwa jambo hilo linakwenda kukamilika na kuondoa mkwamo kwa wananchi.

"Hili kongamano hilo limetukumbusha mambo mengi tumejifunza kutoka nchi zilizopitia mapito kama ya Tanzania lakini tumejifunza namna ya kushinda vikwazo,"Alisema.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Gaudensia Kabaka, alisema chama hicho kitaendelea kushirikiana na vyama vya siasa huku akisema Tume ya uchaguzi iliyopo ni huru isipokuwa kuna mapungufu kidogo.

# Majaliwa asifu mchango wahandisi wanawake

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amesema serikali inatambua mchango mkubwa unaotolewa na wahandisi wanawake katika kuchangia ukuaji wa uchumi nchini.

Majaliwa aliyasema hayo jana wakati akizindua Kongamano la Saba la Wahandisi Wanawake katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam.

"Serikali inatambua umuhimu wa tasnia ya uhandisi kwa ustawi wa nchi nzima, hivyo inahitaji kuhamasishwa na kupewa kipaumbele ikiwa ni pamoja na kutengeneza viongozi wengi zaidi wanawake katika tasnia ya uhandisi. Mheshimiwa Rais (Samia Suluhu Hassan) amekuwa kielelezo cha ubora, maono, uthabiti na uthubutu kwa viongozi wanawake.

"Kupitia uongozi wake, tumeshuhudia namna anavyoifungua nchi yetu ikiwa ni pamoja na kufungua njia kwa wanawake wengi kuwa na uthubutu na kujiamini. Sasa njia iko wazi kwenu, kazaneni na wekeni bidii ili kazi yenu iendelee kuonekana na Taifa lisonge mbele," alisema.

Waziri Mkuu pia alisema amefurahishwa na shughuli mbalimbali ambazo Taasisi ya Wahandisi Tanzania kupitia Kitengo cha Wahandisi Wanawake inajihusisha nazo. Alisema shughuli hizo zimekuwa msaada mkubwa kwa serikali katika kufanikisha azma yake ya kuwafikia Watanzania wote kuhusu kupata elimu ya masuala ya kihandisi.

"Ziara mnazofanya kwenye shule za sekondari na vyuo zimekuwa na mchango mkubwa katika kuandaa kizazi cha baadaye chenye ujuzi na uwezo wa kung'amua mambo mapema kwa maslahi mapana ya ustawi wa nchi. Kitendo hiki pia ni ishara ya umoja uliopo baina yenu kwani mmeonesha uzalendo mkubwa na kwamba muda wote mnaitakia mema nchi yenu," alisema.

Majaliwa alisema serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuhamasisha wasichana katika shule za sekondari wapende na kusoma masomo ya sayansi na hisabati, kutembelea vyuo vikuu ili kuongea na wanafunzi wa kike wanaochukua kozi zinazohusiana na ujenzi na kuwajengea uwezo wanawake ili waweze kusajili kampuni na kufanya kazi za ukandarasi.

"Niwaase kutumia fursa hii kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ili kuongeza ushiriki wa wanawake katika tasnia ya ujenzi. Serikali inatambua mchango wa taaluma ya uhandisi kwa fani mbalimbali katika ukuaji wa uchumi wa Taifa kupitia ufanikishaji na ukuaji wa huduma mbalimbali.

"Kwa takwimu za Machi, 2022 Tanzania ina wahandisi wapatao 30,921 kati yao wanawake ni 3,982 sawa na asilimia 12.88 tu. Hii ni idadi ndogo sana, hivyo tunahitaji kuwa na wahandisi wanawake wengi zaidi, na hii ikiambatana na ongezeko la mafundi sanifu na mafundi mchundo. Serikali inaunga mkono juhudi hizi kwa kuanzisha shule za sayansi kwa wanawake katika kila mkoa," alisema.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi anayeshughulikia Ujenzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, alitoa wito kwa wakandarasi na wahandisi washauri wanawake wafanye kazi kwa uadilifu na kuhakikisha miradi inakamilika kama ilivyopangwa na kwa viwango stahiki.

"Nipende kutoa rai kwa wahandisi wanawake wote wa fani zote za mlengo wa kihandisi mlioko hapa, muendelee kuhakikisha shughuli za ujenzi zote tunazofanya zinafuata taratibu zote za kihandisi na kuhakikisha thamani ya pesa inaonekana katika miradi yote mnayosimamia na kufanya kazi."

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maandalizi Ligi Kuu Bara yaendane na uhitaji halisi

**PAZIA** la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu mpya wa 2022/ 2023 linatarajiwa kufunguliwa rasmi ifikapo Agosti 17, mwaka huu kwa timu zote 16 zinazoshiriki kuanza mbio za kuwania taji hilo linaloshikiliwa na Yanga ya jijini Dar es Salaam.

Yanga ilitwaa ubingwa huo kwa kuwavua watani zao, Simba ambao walikuwa wanaushikilia ubingwa kwa msimu wa nne mfululizo.

Mshindi wa taji hilo na timu inayoshika nafasi ya pili, zinapata tiketi ya kuiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Msimu uliopita, Yanga inayofundishwa na Kocha Mkuu, Nasreddine Nabi, raia wa Tunisia ilitwaa ubingwa huo kwa kuweka rekodi ya kutofungwa, lakini ikijihakikishia ubingwa ikiwa imebakiza mechi tatu mkononi.

Hata hivyo, kazi kwa Yanga haikuwa nyepesi, ilikutana na changamoto mbalimbali katika mbio hizo za kutimiza malengo yake.

Yanga ilipambana katika kila mechi, ikiweka msimamo kwamba kila mchezo kwake ni fainali na kauli mbiu hiyo ilichangia kuongeza morari kwa wachezaji, viongozi, wanachama na mashabiki.

Hata hivyo Yanga haikufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa ya CAF kwa kutolewa kwenye hatua za mapema wakati wapinzani wao, Simba wakiishia hatua ya robo fainali.

Ili kila timu ifike malengo, huu ni wakati wa kuhakikisha zinafanya maandalizi kwa mujibu wa programu zilizoandaliwa na viongozi wa benchi la ufundi.

Mpira wa miguu ni mchezo wa wazi na usiohitaji au usiotegemea miujiza, unatakiwa kuiandaa vyema timu yako ili kutarajia kupata matokeo chanya na si vinginevyo.

Tunapenda kuchukua nafasi hii kuzikumbusha timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi ya Championship, First League na Ligi Kuu ya Wanawake Nchini kufanya maandalizi sahihi ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kupata ushindi na hatimaye kuwania mataji.

Ukiondoa vita ya kuwania ubingwa na kupata tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa, lakini klabu zikumbuke kumaliza kwenye nafasi za juu na hatimaye kuondoka na fedha 'nono' zinazotolewa na mdhamini mkuu, Benki ya Taifa ya Biashara pamoja na Kampuni ya Azam Media inayotoa motisha hadi kwa klabu inayoshuka daraja.

Kama timu zilikuwa zikijiandaa na kufanya usajili wake bila ya kuwa na zawadi hiyo kutoka Azam Media, je sasa zinapopokea fedha hizo, ni vyema viongozi wakazitumia kwa malengo yaliyokusudiwa na si vinginevyo.

Ni wazi timu inayokosa maandalizi, hujiweka katika janga la kukaa mkiani lakini pia kuwa kwenye presha ya kushuka daraja.

Ilishatangazwa dirisha la usajili litafungwa rasmi ifikapo Agosti 31, mwaka huu, tunawakumbusha mwezi mmoja uliobakia utumike vyema kukamilisha mchakato wa usajili lakini wiki mbili kuelekea msimu mpya ukamilishe maandalizi ambayo yanatarajiwa yataimarisha vikosi vyenu.

Ni wazi ubora wa vikosi husaidia kuongeza ushindani kwenye ligi na kumpa nafasi kubwa Kocha wa Taifa Stars, Kim Poulsen, wepesi wa kuteua wachezaji kwa ajili ya timu yake.

Tunafahamu ili maandalizi yafanyike kwa kiwango bora, kiasi kikubwa cha fedha kinahitajika na baadhi ya timu hazina wadhamini wa kusaidia kugharamia huduma hizo muhimu, lakini hilo halihalalishi wasimamizi wa timu kupeleka mambo kwa mazoea.

Wachezaji pia kuweni makini katika kusaini mikataba na timu ambazo hazina uhakika wa kupata nafasi ya kucheza.

Wachezaji mnatakiwa kuwahusisha mawakala au wanasheria wenu nakala za mikataba kabla ya kusaini mikataba ili kujiweka mahali salama na kujiepushia uonevu kwa kuvielewa vyema vipengele vilivyokuwa kwenye mikataba hiyo.

Viongozi wa klabu watendeeni haki wachezaji wenu kwa kuwapa vifaa bora lakini pia kuwalipa haki zao kwa wakati ili akili zao zitulie na kujikita katika mazoezi pekee ili kutorudisha nyuma vipaji vyao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wachezaji wa Kitanzania waanze kujishtukia

Na Adam Fungamwango

**HUU** ni wakati wa usajili ambapo klabu mbalimbali za Ligi Kuu zinasaka wachezaji kwa ajili ya kuwafanyia kazi kwa msimu ujao.

Kuna kitu nimeanza kukiona ambacho si kizuri kwenye mustakabali wa soka la Tanzania. Nacho ni baadhi ya klabu kuacha idadi kubwa ya wachezaji hasa wa Kitanzania.

Pia kwa sasa klabu hata zile zinazoitwa au kujiita ndogo kuanza kushusha wachezaji wa kigeni. Hapa kuna shida mahala.

Kama vile haitoshi nimemsikia Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Almasi Kasongo kukiri kupokea maoni mbalimbali ya wadau wa mpira wa miguu kwa ajili ya maboresho ya kanuni za Ligi Kuu msimu ujao wa 2022/23, huku suala ya wachezaji 12 wa kigeni likiwa miongoni mwa maoni hayo.

Kifupi tu ni kwamba wengi waliopeleka mapendekezo wametaka wachezaji wa kigeni wote wacheze.

Kanuni ya msimu uliopita iliruhusu wachezaji wanane tu kuanza kikosi cha kwanza

"Ndiyo, tumepokea maoni, tofauti kutoka kwa wadau ni klabu, kila mmoja anataka kuonyesha ni namna gani nzuri inatakiwa iwe, lakini maoni mengi yameelekeza wachezaji wa kigeni ikiwezekana wapewe nafasi au fursa ya kucheza wote, lakini kama ninavyosema ni mapema sana bado tupo kwenye huo mchakato, tutapeleka kwenye vikao halali vitaamua kwa sababu hili ni jambo la kanuni siyo jambo la Bodi, wala TFF (Shirikisho la Soka Nchini), ni la wadau wenyewe, ambao ni klabu, wenyewe ndiyo wataamua ni namna gani ambavyo wanataka wachezaji wa kigeni, 12 wacheze wote, au wanane kama ilivyokuwa msimu uliopita, sisi tuko tayari kulingana na mahitaji ya wadau wenyewe ambao wana fursa ya kutumia wachezaji hao na kuwamiliki pia," alisema Kasongo.

Binafsi mimi siyo muumini wa kuwatetea wachezaji wa Kitanzania, eti wapunguzwe wachezaji wa kigeni kwa ajili ya kuwabeba wazawa.

Mimi naamini kuwa kila mchezaji acheze kwa uwezo wake, awe mgeni au mzawa.

Iwapo kanuni hii itapita itakuwa mwiba kwa wachezaji wa Kitanzania ambao hawajitumi, kwani makocha watakuwa wakichagua wachezaji wenye uwezo na wenye kujituma mazoezini.

Hapa sasa ndiyo inatakiwa wachezaji wa kizawa wafanye kazi ya ziada kupambana ili kupata namba.

Hii ni kengele ya hatari inaanza kugonga kwa wachezaji wa Kibongo.

Wakati hii inaweza kuwa mwiba kwa wachezaji wa kizawa hasa wa Simba, Yanga na Azam, ambao ndiyo wenye uwezo kusajili wachezaji 12, huku kwenye klabu ndogo nako naona taratibu hata zile timu ambazo zilikuwa hazichukua wageni kutoka nje, zimeanza kufanya hivyo.

Ina maana kuna sehemu ambapo wachezaji wa Kitanzania hawafanyi vema. Ninaamini, kama wangekuwa wako vema, sidhani kama Mtibwa Sugar, au Coastal Union zingeanza kusajili wachezaji kutoka nje ya nchi.

Tuangalie klabu kama Prisons, Dodoma Jiji na KMC zimeacha wachezaji wengi sana. Ingawa ni kwa sababu mbalimbali, lakini wengi ni kwamba klabu zimewaacha kutokana na kutoridhishwa na viwango vyao.

Kila timu hapo imeacha wachezaji wasiopungua 10. Ukimsikiliza Thobias Kifaru wa Mtibwa na Christina Mwagala wa KMC wameachana na wachezaji hao kutokana na kutokidhi matakwa.

"Unapotaka kujenga timu ni lazima ufanye maamuzi magumu, tumeacha wachezaji wengi kwa sababu tunataka kujenga timu imara." Anasema Mwagala.

"Hao tulioachana nao mikataba yao imemalizika na hatukutaka kuendelea nao, kwa sababu hawa ndiyo waliotufanya kucheza 'play off' kwa misimu miwili mfululizo. Anasema Kifaru.

Hii inaonyesha wengi wameondoka kwa kutoonyesha kipya, na hakuna ubunifu.

Lakini wachezaji hawa hawa wamekwenda kujiunga na klabu zingine. Huyu ametoka huku kwenda huku na huyu ametoka huku kwenda kule.

Ninachowaasa sasa wachezaji wa Kibongo waanze kujitathmini. Wameanza kuonekana ni wa kawaida sana hata kwenye klabu za kawaida. Huko mbele tunakokwenda itakuwa hatari.

Wabadilike na kupambana kwa kuzipigania timu zao. Kutojituma, kuhujumu, na kutopambania timu kinatajwa kuwa ni moja ya sababu ya kutoaminika.

Hii ni nafasi ya mwisho kwao. Haiwezekani straika umalize ligi una mabao matano tu.

Isije baadaye ukazuka mjadala wa kutaka kuonewa huruma huku wenyewe wanashindwa kujitathmini.

# Kiongozi wa Mwenge ashtukia ubora vyumba vya madarasa

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

KIONGOZI wa Mbio za Mwenge Kitaifa, Sahil Geraruma, ametilia shaka mradi wa kwanza wa madarasa mawili katika Shule ya Sekondari ya Mwakata iliyojengwa kwa nguvu za wananchi.

Geraruma alitilia shaka mradi huo baada ya kukuta baadhi ya madarasa yakiwa na nyufa hali ambayo ilimtia wasiwasi juu ya ubora wake.

"Ninawaomba kutokana na hayo njooni kwa muda wenu kuja kurekebisha upungufu huu kwani wananchi wanapokuwa wakitoa nguvu zao katika ujenzi, halmashauri husika haina budi kuwapa moyo kwa kuwasadia wataalamu kwa ajili kujenga kitu chenye ubora," alisema.

Geraruma aliyasema hayo jana baada kuzindua vyumba viwili vya madarasa katika shule hiyo iliyopo Halmashauri ya Msalala na kuwataka wataalamu wa halmashaiuri hiyo kuhakikisha wanakuwa nyuma ya wananchi wakati wa ujenzi wa miradi yao ya maendeleo.

"Mimi ni kijana mdogo lakini nimeaminiwa na Rais, hivyo ninawaomba nyinyi wataalamu angalieni majibu yenu wakati ninapowauliza juu ya utekelezaji wa miradi yenu," alisema.

Kiongozi huyo alieleza pia kusikitishwa na baadhi ya nyaraka za malipo kutokuwapo hali ambayo ilimfanya kuwaonya watumishi hao kuacha tabia ya kutohifadhi nyaraka hizo kwani ni kinyume cha sheria.

Akisoma taarifa ya mradi huo, Mkuu wa Shule hiyo, Gasper Barnaba, alisema ujenzi huo umegharimu Sh. milioni 40 hadi kukamilika kwake hali ambayo itafanya wanafunzi kusoma katika mazingira mazuri. Barnaba alisema awali wanafunzi walikuwa wakitembea umbali mrefu kwenda shuleni kutoka katika maeneo mbalimbali hali ambayo ilichangia wengine kuacha shule, hivyo kutokana na kupatikana madarasa hayo, kutapunguza mwendo wa kutembea.

Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Shinyanga Santiela Kirumba, aliwataka wazazi, kutokana na madarasa hayo kukamilika kujengwa kuhakikisha kuwa wanawapeleka watoto shule ili wapate elimu ambayo itakuwa msaada mkubwa katika maisha yao.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, akipokea mwenge huo kutoka Wilaya ya Kishapu, alisema unatarajia kuzindua miradi 15 yenye thamani ya Sh. bilioni saba na utakimbizwa umbali wa kilometa 308.

Alisema kuwa utakimbizwa katika halmashauri za Ushetu, Msalala, na Manispaa ya Kahama na kufungua miradi mbalimbali ya maendeleo na baadaye kukabidhiwa mkaoni Tabora.




Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (katikati), akikata utepe kuzindua duka la Vodacom linalotembea kwa mikoa ya Kanda ya Kati, jijini Dodoma jana. Wengine ni Mkuu wa Mauzo Vodacom Kanda ya Kati, Joseph Sayi (kushoto), Mkurugenzi Kitengo cha huduma kwa Wateja Vodacom, Harriet Lwakatare (wa pili kushoto), Mbunifu wa duka hilo, Mhandisi Emmanuel Maiga (wa pili kulia) na Mkuu wa idara ya mauzo na usambazaji Vodacom Tanzania Plc, George Lugata. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali kuboresha mfumo utoaji haki

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

NAIBU Waziri wa Katiba na Sheria, Geoffrey Pinda, amesema serikali imekusudia kuimarisha mfumo wa upatikanaji wa haki nchini huku akibainisha kuwa watoa huduma ya msaada wa kisheria ni wadau muhimu.

Ili kufanikisha hilo, Pinda amesema serikali inakusudia kuimarisha utekelezaji wa Sheria ya Msaada ya Mwaka 2017 na kanuni zake za mwaka 2018. Pinda alisema jana wakati akizungumza na watoa huduma ya msaada wa kisheria mkoani Ruvuma iliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea. Zaidi ya watoa huduma ya msaada wa kisheria 50 walishiriki.

Alisema Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na mambo mengine, inaendelea kuboresha upatikanaji wa haki na huduma ya msaada wa kisheria ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua mbalimbali kama kuondoa ada ya usajili wa wasaidizi wa kisheria na kuweka mfumo wa usajili katika ngazi za mikoa na wilaya.

Pia alisema, wizara imeanzisha kamati za uratibu wa msaada wa kisheria kwa mikoa 25 nchini na imeunganisha watoa huduma na taasisi za serikali na mahakama kwa ajili ya shughuli za msaada wa kisheria kwa kuanzisha madawati ya huduma hiyo kwenye vituo jumuishi sita vya utoaji haki katika mikoa ya Dar es Salaam (Kinondoni na Temeke), Arusha, Mwanza na Dodoma.

Alisema serikali pia inaandaa mpango wa kuwa na vituo jumuishi vya sekta ya sheria na ndani ya vituo hivyo, kutakuwa na ofisi za wasaidizi wa kisheria na wadau wote wakiwamo wakisheria tayari wameshirikishwa katika uandaaji wa aandiko linalotarajiwa kutolewa hivi karibuni.

Kaimu Katibu wa Kamati ya Uratibu ya Watoa Huduma za Msaada wa Kisheria mkoani Ruvuma, Rajabu Songambele, alisema kwa muda mrefu wamekuwa wakikabiliwa na ukosefu wa bajeti, hivyo kufanya kazi katika mazingira magumu.

Alisema kutokana na hali hiyo, wameshindwa kumudu kutekeleza yale wanayokutana nayo toka kwa wadau, wakiwamo wananchi ambao wanahitaji msaada wa kisheria.

"Tunaomba utufikishie salamu zetu kwa Rais Samia Suluu Hassani kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kuifanya ya ndani ya nchi yetu ikwamo ya ujenzi wa miundombinu ya barabara, shule za msingi, sekondari, zahanati, vituo vya afya na hospitali," alisema Songambele. Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Mary Makondo, aliwahimiza watoa msaada wa huduma ya kisheria kufanya kazi kwa weledi na wahakikishe wanatenda haki na si kutanguliza maslahi binafsi.

Makondo pia aliwataka kuona umuhimu wa kushiriki sensa ya watu na makazi ambayo inatarajiwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu.

# Wadau madini, gesi waiangukia serikali

**Na Richard Makore, MWANZA**

WADAU wa sekta za madini na gesi wameomba serikali kuweka mfumo utakaosaidia wananchi kupata taarifa za fedha za ushuru wa huduma zinazolipwa na wawekezaji kwenda katika halmashauri mbalimbali nchini.

walisema hayo jana katika warsha ya siku mbili iliyofanyika Jijini Mwanza na kukutanisha wananchi wanaoishi katika maeneo yenye migodi wakiwamo, madiwani wa sehemu hizo, watetezi wa masuala ya mazingira wadau wa utetezi wa raslimali za Taifa.

Akizungumza katika warsa hiyo, mtafiti kutoka shirika la Policy Forum, Eliname John, alisema asilimia 98 ya wananchi katika maeneo yanapochimbwa madini hawashirikishwi kuhusu fedha hizo.

Pia alisema asilimia 65 ya wananchi hao hawajui namna ushuru huo unavyolipwa kwa halmashauri mbalimbali kama sheria inavyotaka.

John alisema kutokana na hali hiyo kuna haja ya mashirika mbalimbali yasiyokuwa ya, serikali na wadau wengine kuendelea kuwajengea uwezo wa elimu wananchi wanaotoka katika mikoa yenye madini ili wajue namna fedha hizo zinavyolipwa.

Alisema wananchi wanahitaji elimu ili kushiriki na kushirikishwa katika shughuli mbalimbali zinazohusiana na sera ya ukusanyaji wa mapato katika sekta ya madini.

Naye Diwani wa Matongo, Tarime mkoani Mara, Felister Range, alisema tatizo la elimu ndogo linachangia wananchi pamoja na madiwani kushindwa kumhoji mkurugenzi wa halmashauri kuhusu fedha hizo.

Alisema licha ya madiwani kupanga bajeti kuhusu maendeleo, mtu wa mwisho anayepeleka taarifa hizo serikalini ni mkurugenzi wa halmashauri jambo ambalo linaweza kumfanya abadilishe kitu walichokubaliana.

"Sisi madiwani tunakutana na kupanga bajeti yetu ya halmashauri ambayo ndani ya mwaka kuna fedha za ushuru wa huduma zilizolipwa na wawekeazaji kwenye migodi, lakini anayepeleka taarifa hiyo Dodoma ni mkurugenzi wa halmashauri, hivyo kuna uwezekano huko njiani akabadilisha walichokubaliana," alisema.

Alikiri kwamba wananchi hawapati nafasi ya kushiriki ama kushirikishwa kuhusu matumizi ya fedha hizo na kwamba kuna haja ya kufanya mabadiliko ya sheria ili kila mtu apate nafasi ya kujua.

Mdau wa madini kutoka mkoani Mara, Boni Mato, alikiri wananchi wengi hawajui kinachoendelea kuhusiana na fedha hizo, na kwamba kuna haja kwa serikali kuu na serikali za mitaa kutoa elimu.

Alisema mipango yote inapangwa na mkurugenzi wa halmashauri kama katibu wa baraza la madiwani akishirikiana na madiwani, lakini wananchi hawajui chochote.

Aidha, alisema kuna haja ya kubadilisha sheria ili kuweka vigezo katika elimu ili mtu aweze kugombea udiwani lengo likiwa ni kupata wawakilishi wa wananchi wenye uelewa.

"Katibu wa baraza la madiwani ni mkurugenzi wa halmashauri ambaye amesoma. Madiwani wengine hawajui hata kusoma na kuandika sasa wanawezaje kupanga mipango yao pamoja na ikabaki kama walivyokubaliana," alihoji Mato.

Warsha hiyo iliandaliwa na shirika la Hakiraslimali kwa lengo la kupata maoni ya wadau mbalimbali wanaotoka mikoa yenye migodi ili kujua namna fedha za ushuru wa huduma zinavyosaidia maendeleo ya wananchi.

## HABARI KITAIFA

## DC ahamasisha chanjo UVIKO- 19

**Na Steven William Iringa**

MKUU wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, ameanzisha kampeni ya uhamasishaji chanjo ya UVIKO- 19 kutokana na kuwapo kwa mazingira ya baridi ambayo ni kichocheo cha ugonjwa huo.

Moyo aliyasema hayo juzi wakati akiwaeleza wananchi wa kata ya Magulilwa katika kikao cha uhamasishaji wa kampeni hiyo.

Akiwa katika kampeni hiyo kwenye Vijiji vya Magulilwa na Ndiwili, alisema wananchi wanapaswa kuchukua hatua kujikinga na ugonjwa huo hasa katika majira haya ya baridi, ambayo ugonjwa huo hujitokeza na kugharimu maisha ya watu.

Licha ya kujikinga, mkuu huyo wa wilaya aliwataka wananchi kujitokeza kupata chanjo ya UVIKO-19, hivyo kujiweka katika mazingira mazuri ya kuwa na kinga dhidi ya ugonjwa huo.

Mkuu huyo wa Wilaya aliwaagiza Wenyeviti wa Vijiji, viongozi wa kata, Madiwani na Maofisa Watendaji kuhakikisha wanawahamasisha wananchi kujitokeza kuchanja kwa kuwa huduma hiyo ni bure.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwajali wananchi wake, amewezesha serikali kupata mkopo kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa ajili ya kununua chanjo, hivyo inatakiwa kumuunga mkono kuchanja.

Kutokana na hamasa hiyo, baadhi ya wananchi walimpongeza Mkuu wa Wilaya kwa kuanzisha kampeni hiyo huku wakieleza kuwa wameipokea kwa mikono miwili.

# TANESCO yawaangukia madereva bajaji, bodaboda ulinzi miundombinu

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Singida limewataka madereva wa bajaji na pikipiki kutoa taarifa mbalimbali pale wanapoona matukio ya uharibifu wa miundombinu ya umeme katika maeneo wanayopita. Ofisa Uhusiano na Huduma kwa Wateja wa TANESCO Mkoa wa Singida, Rehema Mwaipopo, alitoa rai hiyo juzi alipokuwa akizungumza na madereva hao kwa lengo la kuwaomba kuwa mabalozi wao ambao watakuwa wakitangaza huduma zinazotolewa na shirika hilo.

Mwaipopo alisema kumekuwa na tabia ya watu wasio waaminifu kung'oa vyuma kwenye nguzo za umeme mkubwa kwa ajili ya kutengenezea mikokoteni ya kukokotwa na ng'ombe na matumizi mengine kama kutengeneza mapanga na zana zingine.

Alisema wameamua kushirikiana na madereva hao kutokana na wingi wao na huduma wanazozitoa ambapo kila siku wanakutana na watu, jambo ambalo litasaidia kwa kiasi kikubwa kutangaza huduma za TANESCO.

Kutokana na ushirikiano huo, alisema TANESCO itawaunganisha katika mfumo ambapo watakuwa wakipata ujumbe kwenye simu zao ambao utakuwa na taarifa mbalimbali zikiwamo za kukatika kwa huduma na umeme na wao watawajulisha wateja wanaowabeba.

Mwaipopo alisema msimu wa kilimo unapoanza kumekuwa na kazi ya kusafisha mashamba ambayo yapo chini ya nguzo za umeme hivyo wakati wa kazi hiyo wananchi wanatakiwa wasichome moto kwani wanaweza kusasabisha hatari.

Aliwataka madereva hao kuwa mabalozi wa kutoa maelezo kwa watumiaji wa vyombo vya moto kutoegesha vyombo vyao chini ya nguzo za umeme na transfoma kwani kunaweza kuhatarisha usalama wa wananchi na vyombo hivyo vya moto. "Ninyi sasa ni mabalozi wetu jambo lolote mtakaloliona haliko sawa huko mnakoishi na kupita linalohusu umeme, tujulisheni. Pia kama kutakuwa hakuna matumizi ya vifaa vinavyotumia umeme kama pasi, majiko, majokofu, taa na vingine mvizime pia waambieni na wananchi wengine mnaoishi nao na wale mnaowabeba kwenye vyombo vyenu," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Madereva na Wamiliki Pikipiki na Bajaji Tanzania (CHAMWAPITA) Mkoa wa Singida, Ahmed Mohamed, alitumia nafasi hiyo kulishukuru shirika hilo kwa kufadhili mkutano na kuratibu mpango huo ambao ni muhimu kwa wananchi ambapo kama mabalozi ameahidi watatoa ushirikiano wa hali na mali ili kufikia malengo.

Mikakati hiyo mipya imekuja baada ya TANESCO Mkoa wa Singida kupata meneja mpya, Mhandisi Florece Mwakasege, aliyehamishiwa mkoani hapo hivi karibuni akitokea mkoa wa Ruvuma.




Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (katikati), akikata utepe kuzindua duka la Vodacom linalotembea kwa mikoa ya Kanda ya Kati, jijini Dodoma jana. Wengine ni Mkuu wa Mauzo Vodacom Kanda ya Kati, Joseph Sayi (kushoto), Mkurugenzi Kitengo cha huduma kwa Wateja Vodacom, Harriet Lwakatare (wa pili kushoto), Mbunifu wa duka hilo, Mhandisi Emmanuel Maiga (wa pili kulia) na Mkuu wa idara ya mauzo na usambazaji Vodacom Tanzania Plc, George Lugata. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki ya NBC yazindua malipo mapya mtandaoni

**Na Joseph Mwendapole**

BENKI ya NBC imezindua kadi inayowezesha malipo mtandaoni kwa njia ya Dola na kupitia kadi hiyo wateja wanapata fursa ya kufanya malipo ya bidhaa na huduma kwa dola pasipo makato ya ziada.

Hatua hiyo ni mapinduzi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) yanayowezesha malipo ya 'visa card' inayohakikishia wateja usalama na urahisi pindi wafanyapo malipo ya mtandao.

Mkurugenzi Msaidizi wa NBC, Elibariki Masuke, alisema lengo kuu ni kuhakikisha wateja wao wanazifikia fedha zao kiusalama na wanakuwa na uwezo wa kufanya miamala kwa urahisi, kuboresha huduma zao.

"Kadi hii ni haraka, rahisi kutumia na salama, njia bora kabisa ya kufanya malipo na miamala ya kimtandao. Kadi hii inaondoa kero ya kubana fedha nyingi kwani hali hiyo huhatarisha usalama wa fedha.

"Tunayo furaha, kuzindua kadi hii ya malipo ya visa ya fedha za kimarekani,ambapo itaongeza ufanisi kwa wateja wetu na kuwezesha urahisi wa kufanya malipo na miamala ya dola za kimarekani," alisema.

Kwa kuzingatia matumizi na usalama, Masuke alisema kadi hiyo ya malipo ya visa ya dola za Kimarekani ni rahisi na salama kwa kuwa zinalindwa na teknolojia ya 3D chip na pini za kisasa.

Mbali na kumwezesha mtumiaji wa kadi hiyo kufanya malipo ya mtandaoni bila malipo ya ziada, alisema kadi hiyo pia ina uwezo wa kutumika kwenye kampuni za Visa zaidi ya 2000 (ATM) kwa Tanzania, zaidi ya kampuni milioni 2.7 za Visa duniani kote na zaidi wafanyabiashara 24,000 wanaopokea malipo ya Visa kwa Tanzania.

Mkurugenzi wa Kadi za Benki ya NBC, Esnat Hollela, alisema kadi hiyo inatumia malipo ya fedha za dola za Kimarekani pia ina uwezo wa kulipia huduma kwa fedha zingine.

"Kwa malipo ya mtandao na tovuti, kadi hii inauwezo wa kufanya malipo yote ya kimtandao kama vile,Amazon, AliExpress, Alibaba na kununua vifurushi kama vile Netflix, DSTV na malipo mengine ya mtandao," alisema.



# Simbachawene ataka Padri Wissi aenziwe kwa kutunza mazingira

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Uratibu na Sera, Geogre Simbachawene, ameongoza mamia ya watu kwenye maziko ya aliyekuwa Makamu wa Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dodoma, Padri Onesmo Wissi, na kuhimiza kumuenzi kwa kutunza mazingira.

Maziko hayo yalifanyika juzi katika makaburi ya Mtakatifu Maria Imakulata Bihawana Jijini Dodoma.

Akizungumza kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan, alisema Padri Wissi atakumbukwa kwa utendaji kazi wa kueneza neno la Mungu.

Pia alisema, kwa niaba ya Rais anatoa pole kwa waumini wote pamoja na kanisa huku akisisitiza kuwa Padri Wissi, ameondoka wakati kanisa linamhitaji lakini yote hayo ni mapenzi ya Mungu.

"Padri Wissi ameondoka akiwa bado tunamhitaji kwenye utoaji wa huduma za kiroho lakini hatuwezi kupingana na kazi ya Mungu," alisema Simbachawene.

Naye Askofu Mkuu wa kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dodoma, Beatus Kinyaiya, alisema waumini na watu wote kwa ujumla wanapaswa kumuenzi aliyekuwa marehemu kwa kutunza na kuyahifadhi mazingira kama alivyokuwa akifanya wakati wa uhai wake.

Askofu Mkuu Kinyaiya, alisema Padri Wissi enzi za uhai wake alikuwa mtu wa kutunza mazingira na kuyahifadhi. "Mazingira ni mama yetu hasa hapa tunapokuwa duniani mazingira hivyo, tunahitaji kutunza mazingira na kuheshimu, Padri Wissi alifanya mazingira yapendeze na kuifanya nyumba ya Mungu ipendeze pia," alisema Askofu Mkuu Kinyaiya.

Pia alisisitiza kuwa waumini na watu wote wenye mapenzi mema popote wanapokuwapo kamwe wasichafue mazingira kwa kutupa, hovyo taka, kukata miti, kuharibu vyanzo vya maj,i na mazalia ya viumbe maji kwa kuwa hiyo ndiyo kazi aliyopewa kila mtu na Mwenyezi Mungu.

Pamoja na suala la Utunzaji Mazingira, Askofu Kinyaiya alitoa wito kwa jamii kuweka utamaduni wa kupima afya zao mara kwa mara na hasa watu wazima wenye umri kuanzia miaka 50 na kuendelea.




Naibu Meya wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma aliyemaliza muda wake, Emmanuel Chibago (kulia), akizungumza na madiwani wa halmashauri hiyo, baada ya kukabidhi nafasi hiyo kwa Naibu Meya aliyechaguliwa, Jamal Ngalilya (kushoto), jijini humo juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Serikali, kampuni ya Uingereza zaingia mkataba kuandaa kongamano TEHAMA

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, imetia saini mkataba wa maridhiano na Kampuni ya EXNTENSIA ya Uingereza ili kuandaa kongamano la masuala ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) nchini.

Kongamano hilo litakuwa na lengo la kutoa nafasi ya majadilinao baina ya wadau wa TEHAMA nchini na kampuni zinazoajihusisha na masaula hayo kutoka nje ya nchi ili kubaini fursa na vikwazo vilivyopo katika sekta hiyo nchini.

Akizungumza baada ya kutia saini mkataba huo juzi jijini hapa, Katibu Mkuu Wizara hiyo, Dk. Jim Yonazi, alisema kongamano hilo litasaidia kuchangia uchumi wa kidigitali na litawaleta wadau mbalimbali wenye nia ya kuwekeza katika TEHAMA.

"Wadau watakuja kujifunza nchini kwetu na kongamano hilo tunatarajia kufanyia Septemba 7 na 8, mwaka huu, na linatarajiwa kuwa na wageni takribani 300 watakaokuja kujifunza na hawa watakuja kukutana na wananchi wenye nia ya kuwekeza katika TEHAMA na tunatarajia kuwa na aina nyingi ya watu waliobobea katika sekta hiyo," alisema Dk. Yonazi.

Alisema Tanzania ina mpango wa kuwa nchi kitovu cha masula ya TEHAMA na ubunifu katika eneo la nchi za Afrika Mashariki na Kati kwa kuwa ni nchi inayounganisha mkongo wa taifa.

Naye Mkurugenzi wa TEHAMA kutoka wizara hiyo, Mulengwa Munaku, alisema kongamano hilo litafanyika Jijini Dar es salaam na litahudhuriwa na mashirika makubwa likiwamo shirika linalosimamia mawasiliano duniani.

"Pia watakuwapo watu wa taasisi wanaosimamia mawasiliano Afrika na hii itakuwa fursa kwa Watanzania kuwekeza hapa nchini kwa lengo la kuongeza ajira," alisema Mnaku.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema mkongo wa taifa ni nguzo muhimu katika kujenga uchumi wa kidigitali.

# Mpango kabambe kuongeza maziwa

**Na Valentine Oforo,** MPWAPWA

WAKALA wa Mafunzo ya Mifugo (LITA) katika Kampasi ya Mpwapwa mkoani Dodoma, inatekeleza mpango wa kuboresha mradi wa ng'ombe na uzalishaji wa maziwa ili kuongeza kipato na kukabiliana na tatizo la ajira kwa vijana.

Katika mpango huo, kufikia Juni, mwakani, chuo hicho kinalenga kuongeza idadi ya ng'ombe wa maziwa wenye tija kutoka 43 hadi 70 na kila ng'ombe kuwa na uwezo wa kuzalisha angalau lita 15 za maziwa kwa siku.

Mpango huo muhimu ulibainishwa jana na Kaimu Meneja wa Chuo hicho, Fredrick Karumuna, kwenye mahafali ya chuo hicho. Wanafunzi 215 walihitimu ngazi ya stashahada ya afya na uzalishaji wa wanyama.

"Mradi huu ni miongoni mwa programu nyingi za ujasiriamali ambazo tunaziendesha chuoni kwa lengo la kukuza kipato, vilevile programu zinazoendelea zinatumiwa na wanafunzi kama jukwaa muhimu la kuweka maarifa yao ya kinadharia katika vitendo," alisema.

Karumuna aliitaja baadhi ya miradi ya kiuchumuni inayotekelezwa na chuo kupitia nguvu kazi ya wanafunzi kuwa ni pamoja na usindikaji wa maziwa na nyama, pamoja na uzalishaji wa malisho bora. Pia alisema chuo kimejikita kutoa elimu bora ya mifugo na inayokidhi vigezo vya kuwawezesha wahitimu kujiajiri, na siyo kubaki majumbani wakisubiri nafasi za kuajiriwa.

"Tunatoa mafunzo yetu kupitia kauli mbiu ya 'Jiajiri, Ajiri, Ajiriwa (JAA). Lengo kubwa ni kuwawezesha wahitimu kukabiliana na changamoto ya uhaba wa ajira katika mfumo rasmi," alisema.

Naye Meneja wa Huduma kwa Wateja wa Benki ya NMB Tawi la Mpwapwa, Martino Somba, aliwataka wahitimu kuchangamkia fursa mbalimbali zinazotolewa na taasisi hiyo ya fedha, ikiwamo mikopo ili kujikwamua kiuchumi kupitia utaalamu waliofundishwa chuni hapo.

Alisema benki hiyo kupitia mpango wake wa ujasiriamali unaofahamika kwa jina la 'Go na NMB', inatoa fursa kwa vijana wa kizalendo kupeleka mawazo yao chanya ya bunifu za miradi ya kiuchumi na ujasiliamali kwa lengo la kupata mikopo ya mitaji.

"Mnayofursa kubwa na adhimu ya kutumia programu yetu ya 'Go na NMB' kufikisha mawazo yenu ya bunifu mbalimbali ili muweze kupatiwa mikopo rafiki ya kuwawezesha kujikita katika miradi binafsi, na hivyo kuondokana na changamoto ya ukosefu wa ajira," aliwaasa.





Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Idrissa Kitwana Mustafa (kulia), akiandaliwa kwa ajili ya kuchangia damu wakati wa uzinduzi wa maadhimisho ya mwaka mpya wa Kiislamu (1444 Hjr) kwa watu mbalimbali waliochangia, katika Mnara wa kumbukumbu Kisonge Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwinyi afurahishwa utekelezaji miradi

**Na Rahma Suleiman,** PEMBA

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema ziara yake imekuwa na mafanikio makubwa kwa sababu miradi yote ya maendeleo aliyotembelea iko vizuri kasoro mradi mmoja tu ambao ujenzi wake umechelewa.

Aliyasema hayo juzi katika ukumbi wa kiwanda cha makonyo, Wawi mkoa wa Kusini Pemba, wakati akifanya majumuisho ya ziara yake ya kutembelea miradi ya maendeleo katika mikoa yote mitano ya Unguja na Pemba.

Dk. Mwinyi alisema miradi aliyotembelea ikiwamo ya afya, elimu na maji iko vizuri na ameridhika na hatua iliyofikiwa na kuwapongeza wasimamizi vikiwamo vikosi vya ulinzi na usalama vya serikali ya Zanzibar vilivyopewa jukumu la kutekeleza miradi hiyo.

Alisema amefurahishwa na mipango ya maendeleo ya mkoa wa Kusini Pemba kutokana na maono ya mkuu wa mkoa huo kuleta maendeleo kupitia miradi inayoendeshwa na mamlaka za mikoa na wilaya.

Mipango na miradi mbalimbali wanayoitekeleza, alisema ndicho ambacho anataka kukiona na kumwahidi mkuu wa mkoa huo kuwa atamsaidia ili kutimiza miradi hiyo katika kuwaletea maendeleo wananchi.

Dk. Mwinyi alirejea kauli yake kwamba bado halmashauri za wilaya, mabaraza ya miji na mabaraza ya manispaa Unguja na Pemba hayajafanya vizuri katika kutekeleza miradi ya maendeleo, hivyo yanatakiwa kuongeza juhudi.

"Uafadhali upo kwa sababu mara ya mwisho nilipokuja Pemba mlikuwa chini kwenye miradi ya maendeleo. Kuna asilimia sita angalau sasa hivi tumefika asilimia 20 lakini bado nataka twende juu zaidi. Nikija tena Pemba tuje maalum kwa kufanya ziara ya miradi iliyofanywa na mabaraza ya miji," alisema Dk. Mwinyi.

Rais Mwinyi alizitaka halmashauri, mabaraza ya miji na manispaa kuongeza bidii angalau kufikia asilimia 30 ya makusanyo ya ndani ili yaende kwenye miradi ya maendeleo.

Pia alisema lazima kufanya kazi ya ziada katika upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama Unguja na Pemba kwa sababu bado upatikanaji wa huduma hiyo ni mdogo na ni wastani wa asilimia 50.

"Tutakaa chini kuangalia njia mbadala ili kuondoa tatizo la maji Unguja na Pemba badala ya kutegemea fedha za bajeti ya serikali," alisema.

Akizungumza wakati Dk Mwinyi akitembelea miradi ya maendeleo, Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Dk. Khalid Salum Mohamed, alisema utekelezaji wa wizara hiyo ni vipaumbele ambavyo ni kuimarisha huduma za kisiwa cha Pemba.

Dk. Khalid alisema utafiti uliofanywa unaonyesha ujenzi wa bandari ya Mkoani katika kiwango cha kimataifa, utaifanya Pemba kuwa lango kuu la kiuchumi wa nchi jirani za bara la Afrika.

## Mkuu wa Mkoa ahamasisha uchangiaji wa damu

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Idrisa Kitwana Mustafa, amewataka wananchi kujitokeza kuchangia damu ili kuokoa maisha ya watu katika jamii.

Akizungumza baada ya kuchangia damu katika Mnara wa Kumbukumbu Kisonge mjini Zanzibar ikiwa ni shamrashamra za kuadhimisha mwaka mpya wa kiislamu, alisema kuchangia huduma hiyo ni muhimu na taifa lina uhitaji mkubwa wa damu, hivyo ni vyema jamii ikahamasika katika jambo hilo.

Idrisa alisema kumekuwa na upungufu wa damu katika baadhi ya vituo vya afya jambo ambalo linahatarisha maisha ya watu, hivyo kuchangia damu kutasaidia kuokoa uhai wa wananchi.

Mkuu huyo aliishukuru Ofisi ya Mufti Zanzibar, kwa kuandaa uchangiaji damu kwa sababu ni jambo jema la kuimarisha afya za wagonjwa na kuweka kumbukumbu za mwaka mpya wa Kiislamu wenye kuleta manufaa kwa jamii.

Naye Sheikh Hassan Othman Ngwali, kutoka Ofisi ya Mufti Zanzibar, alisema wameamua kusherehekea Mwaka Mpya wa Kiislamu kwa kuchangia damu ili kuisaidia jamii kutokana na kuwa na uhitaji mkubwa wa damu katika vituo vya afya.

Alisema jambo hilo ni la kwanza ambalo limeanzia katika mkoa wa Mjini Magharibi na litakuwa endelevu katika mikoa yote ili wananchi kuwa tayari kuchangia damu.

# Makamu wa Rais ashauri mageuzi sekta ya elimu yazingatie ubunifu

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar , Othman Masoud Othman, amekishauri kikosi kazi kinachokusanya maoni ya wadau kuhusu mageuzi ya sekta ya elimu nchini kufikiria kwa mapana zaidi na kuelekeza mtazamo wa mwelekeo wa dunia unaozingatia suala la ubunifu na uvumbuzi wa teknolojia katika maendeleo ya elimu.

Othman aliyasema hayo jana ofisini kwake, Migombani mjini Zanzibar, alipokutana na kikosi kazi kinachokusanya maoni ya wadau kuhusu mageuzi ya sekta ya elimu Zanzibar kinachoongozwa na Makamu Mkuu Mstaafu wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Prof. Ahmada Rai.

Alisema kutokana na mwelekeo wa dunia ulivyo, ni muhimu kufahamu mahali na uwezo wa wananchi kitaaluma sambamba na kujua matarajio ya unapohitaji kufikia katika mageuzi hayo ili kufanya uwekezaji wa maeneo muhimu yanayohitajika.

Kwa mujibu wa Othman, hatua ya kufikiri mageuzi hayo ni kuwa na maono ya kufahamu kwamba elimu itakayofundishwa katika ngazi mbalimbali ina uwezo wa kuzalisha wataalamu wa fani tofauti watakaofanya kazi kwa ujunzi na maarifa makubwa na kushindanishwa na wataalam wanaotoka sehemu yoyote duniani.

Alitolea mfano wa mwalimu atakayezalishwa kwenye vyuo vya Zanzibar kufikiria mageuzi ya kumwandaa mwanafunzi ambaye atafundisha na kukubalika kiuwezo katika nchi yoyote duniani.

Pia alisema kuna haja pia ya kuzingatia kwa makini suala la matakwa ya kitaaluma kwa waajiri wa sekta mbalimbali za maendeleo ikiwamo sekta binafsi kwa kuwa ndio watumiaji wakubwa wa wataalamu wanaozalishwa ndani na nje ya nchi.

Alisema kwamba mwelekeo wa megeuzi unaohitajika pia ni kuwajenga walimu kiuwezo, heshima na maslahi kwa kuwa bila kufanya hivyo, taifa haliwezi kusonga mbele.


Othman pia alikitaka kikosi kazi kuutumia uzoefu uliotumika katika sekta zingine ili usaidie kutoa mweleko juu ya mabadiliko muhimu yanayohitajika ambayo yatachangia kuleta mageuzi stahiki katika sekta ya elimu.

Aidha, Othman alishauri kuangaliwa suala la wajibu na jukumu kwa mzazi katika kuchangia maendeleo ya elimu kwa mtoto ili shughuli ya upatikanaji wa elimu kwa mtoto iwe jumuishi.

Naye Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Abdulghulam Hussein, alisema kikosi hicho chenye wataalamu mahiri kimeaminiwa na serikali na kimepewa jukumu kubwa la kupendekeza mbalimbali za mageuzi yanayohitajika katika sekta ya elimu nchini.

Kwa upande wake, Prof. Ahamada alisema kikosi kimeanza kukutana na wadau katika kuendeleza kazi ya kukusanya maoni ya kupendekeza mageuzi makubwa yanayohitajika katika elimu Zanzibar.

Alisema azma ya serikali ya kutaka kuleta mageuzi katika elimu Zanzibar ni kutokana na changamoto zilizoko ndani ya mfumo wa elimu Zanzibar na kwamba tayari wamejifunza mfumo uliopo sasa kupitia vikao na wadau kabla ya kuwasilishwa serikalini.



## HARMOBOY TZ

UKURASA 12

Nipashe MWANGA WA JAMII
BT
JUMAMOSI JULAI 30, 2022



# UPO NYONYO!

## Sarafina kammaliza Harmonize kila kitu

MASHABIKI wa muziki wa Bongo Fleva, watarajie kuona utamu wa ngoma inayotarajiwa kutoka hivi karibuni inayowashirikisha mastaa Harmonize na Sarafina.

Wanamuziki hao ambao wamekuwa gumzo wanakuja na projekti yao ya kuurudia wimbo wa Sarafina 'Upo Nyoyo' na tayari Harmonize ameshatumiwa mapigo bado kuweka sauti.

Kolabo hiyo imetokana na Harmonize mwenyewe kuuzimia wimbo huo kiasi kwamba akaandika kwenye mtandao wake wa kijamii wa Instagram kuwa anapenda sana ngoma hiyo na kuomba kufanya marudio 'remix', kuimba pamoja na msanii mwenye ngoma yake, Sarafina.

Ngoma hiyo iliyotoka Juni 10, imekuwa gumzo na kutokea kupendwa na mashabiki wengi wa muziki wa bongo fleva kiasi cha staa huyo kumuomba mwanadada kupiga naye kolabo.

Kama ilivyotegemewa, Sarafina hakulaza damu.

"Nimeshamtumia siku nyingi 'beats' za wimbo huo kwa hiyo kila kitu tayari." Anasema Sarafina, na kuwataka mashabiki wa muziki huo siku si nyingi watarajie kufyatuliwa remix hiyo.

Kuhusu baadhi ya mashabiki kudai anaiga uimbaji wa Vanessa Mdee, msanii huyo akasema yeye kwake ni poa tu, kama anaambiwa anamuiga msanii mkubwa kama huyo.

"Kama kuna mtu anasema hivyo kwa kuniponda hiyo ni juu yake, lakini mimi ni msanii mdogo, kufananishwa na yule kwangu ni fahari kubwa. Amekuwa kwenye muziki kwa muda mrefu, wengi wangependa kuwa kama yeye, na mimi nimejifunza vitu vingi kutoka kwake," alisema Sarafina.

BASI SAWA

## Jonathan Budju sasa ni 'Hosanna'



BAADA ya kufanya vizuri na wimbo, Tawala, staa wa muziki wa Injili kutoka nchini Canada, Jonathan Budju, maarufu kama Son Of God, amerudi kivingine na Hosanna.

Akizungumza na BT, Jonathan alisema anashukuru mapokezi yamekuwa makubwa sana katika ukanda huu wa Afrika Mashariki huku wimbo Hosanna ukiingia kwenye chati mbalimbali za muziki.

"Wimbo Tawala ulinipa mashabiki wengi, naamini Hosanna utafanya vizuri zaidi sababu tangu nimeuachia nimeona mapokezi yamekuwa makubwa kwenye mitandao ya kuuza na kupakua muziki hasa YouTube, nawaomba watu wangu wa Afrika Mashariki waendelee kunipa sapoti ili nifike mbali," amesema Jonathan.

## Jay Bonge huyooo wazazi CCM

OMARY Hassani Lihoka maarufu kama Jay Bonge ambaye ni mwigizaji amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Kata ya Kipawa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na BT baada ya uteuzi huo uliofanyika juzi, Jay Bonge alisema anamshukuru Mungu kwa kumpa nafasi hiyo na amepanga kuitumikia kwa uzalendo na uadilifu mkubwa.

"Nimechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi. namshukuru Mungu, nitaitumikia kwa uzalendo na uadilifu mkubwa kutokana na mahali hapa ni sehemu ya chimbuko la wasanii ambao tumewalea na kuwaweka sehemu walizonazo sasa," amesema.





## Ney wa Mitego hebu msikie Harmoboy Tz

RAPA chipukizi Harmoboy Tz, anatamani kufanya kazi na wakongwe wa muziki huo akiwamo Ney wa Mitego na Baba Levo ili kumjengea ujasiri.

Harmoboy Tz ambaye jina lake halisi ni Maneno Paschal, amesema anafuatilia kwa makini kazi za wasanii hao na kufafanua kwa sasa anatamba na nyimbo kama Umama, Tunaishi nao, Wanapagawa, Hunitishi na Utapasi kiatu, ambazo zinasikika katika vituo mbalimbali vya redio na televisheni. Rapa huyo amesema, kwa kuwa ana ndoto ya kufika mbali kupitia muziki wa kizazi kipya, anaamini itatimia iwapo atapata wasanii wakubwa wa kumuunga mkono kwa kukubali kurekodi naye nyimbo zake.





## Talenti Uwezo amlilia 'Afande' amwachie

MWANAMUZIKI anayekuja kwa kasi katika muziki wa Singeli, Iddy Msingi maarufu 'Talenti Uwezo' ametambulisha singo yake mpya inayoitwa 'Afande' ambayo tayari inasikika katika vituo mbalimbali vya redio.

Akizungumza na BT, amesema wimbo huo unaelezea maisha yake halisi ambayo kipindi cha nyuma alipitia changamoto ya kukamatwa na polisi na kuwekwa mahabusu.

"Nikiwa kule nilikuwa nawashawishi polisi wanitoe, ndipo nikapata wazo la kutunga wimbo ambao mashabiki wameonekana kuupokea vizuri," amesema Talenti Uwezo.

Talenti Uwezo tayari anatamba na nyimbo zingine mbili za Kidawa na Sielewi ambazo zote zinaendelea kusikika na kufanya vizuri.

# Sauna: Majanga ya mke wa kurithi

**Na Adam Fungamwango**

KUNA mila za Kiafrika ambazo bado zinaendelea kufuatiliwa na ni nzuri kwa sababu zinautambulisha utu na heshima ya mtu, lakini zipo zilizopitwa na wakati.

Hapa leo tutaiangalia filamu ya 'Sauna', ambayo inamhusu jamaa mmoja aliyepewa mke wa marehemu kaka yake, lakini kilichokuja kutokea ni msukosuko kwenye familia yake.

Wakati mwingine hao wanapewa wake za marehemu wakakuwa na wachumba zao ambao wameahidiana kuona, hivyo kunakuwa na mvutano, kisasi na mambo mengine yanayofanana na hayo.

Imechezwa na wasanii wengi sana, kina Walykister Michael, Salum Nambende, Rikia Mkalomba, Aloyce Joseph, Cauthly Amir na wengineo wengi.

Nambende ana mpenzi wake Zakia ambaye waliahidiana kuwa wataoana. Hata hivyo mipango si matumizi.

Kaka yake anafariki, hivyo ndugu na wazee wanataka amrithi mkewe. Pamoja na Nambende kukataa, lakini anaambiwa mila ndivyo zilivyo, hivyo hakuna atakachoweza kubadili.

Kabla ya kutekeleza hilo anakwenda kumwambia mpenzi wake Zakia. Inakuwa ni huzuni kubwa kwa mpenzi wake, kwani analia na kuona ndoto zote walizopanga zimepotea. Nambende anamrithi mke wa kaka yake na katika ndoa yao, wanabahatika kupata mtoto aitwaye Sauna.

Sauna anakuwa msichana, lakini Zakia bado alikuwa na lake rohoni. Bado alimpenda Nambende na alikuwa hajakata tamaa ya kutaka kuolewa naye.

Anakwenda kwa mganga na kupewa vitu ambavyo vingeweza kumsaidia kuifanya ndoa ya Nambende na mkewe isambaratike.

Pamoja na kwamba Nambende ameoa, lakini mapenzi yao yanaonekana kuwa yalikuwa yanaendelea kama kawaida.

Kuna siku walikutana sehemu na Zakia akamweleza mpenzi wake kuwa mkewe na



binti yake ni wachawi.

Nambende akaonekana kupinga kitu hicho, lakini mpenzi wake anampa uthibitisho na kumwambia aende kwa mganga ili akathibitishe hilo.

Nambende na rafiki yake wanakwenda huko, na wanaambiwa kama Zakia alivyosema. Ina maana Zakia tayari ameshaongea na mganga kuhusu kitu hicho.

Kilichotokea ni kwamba wanapewa dawa ili wakampe mtu fulani. Wanapofika njiani wanakutana na mtu huyo. Wanampa dawa ambayo wamepewa na mganga. Hata hivyo walivyompa tu, mtu huyo aligeuka kuwa Sauna.

Baada ya hapo Sauna hakuwa tena kama mtu wa kawaida, bali kama nusu binadamu na nusu mzimu.

# MAKOSA MA 5 FILAMU ZA KIBONGO

**Na Adam Fungamwango**

KUMEKUWA na ongezeko kubwa la Wabongo kuangalia zaidi tamthilia za Kihindi, Kikorea, Kifilipino na hata Kichina. Kwenye filamu wanaangaliza zaidi za Kizungu, Kichina, Kinaigeria na Kihindi.

Wapo wanaoangalia tamthilia za Kitanzania ambazo nazo zinaonekana angalau zenyewe zinafanya vizuri, lakini kumeonekana kushuka kabisa biashara ya filamu.

Ndiyo maana mastaa wengi wa Bongo Movie wengi wao sasa wanacheza tamthilia. Zipo sababu nyingi za kushuka kwa mauzo ya filamu, na Watanzania kutopenda tena kuziangalia tena.

Ni kwa sababu tayari wameshaonja tamthilia kutoka nje ya nchi, hasa zilipoanza kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Wabongo wameanza kuona aina tofauti ya uigizaji, wenye uhalisia wa hali ya juu, pamoja na uandishi wa hadithi wenye upeo wa hali ya juu. Visa na mikasa wanavyoviona ni vile ambavyo vipo kwenye jamii, japo imetofautiana mazingira kutokana na nchi husika.

Huku kwetu filamu nyingi zinafanana sana. Ni lazima mtu akitoka kijijini masikini lazima awe tajiri, au aoe au aolewe na mtu tajiri.

Mapungufu yaliyo kwenye filamu za Kibongo yanasababisha Watanzania wenyewe kutoridhishwa na jinsi wanavyoigiza.

Leo nitaanza na makosa matano yanayofanywa na filamu za Kibongo, na wiki ijayo pia nitaendelea kuweka makosa mengine ambayo hayakutakiwa kuwepo, au yapo kwa sababu za kimazoea, pia udhahifu wa waongozaji pia.

### Kila mlinzi lazima awe 'chale'

Hii imekuwa kama utamaduni kwenye filamu zetu. Na sijui nani ameanzisha. Na waongozaji wa filamu wote wamekariri. Eti mlinzi wa getini ni lazima awe kama vile zimemruka hivi.

Ukiangalia filamu nyingi, utakuta walinzi wa getini wanakwenda wasanii wa vichekesho, au watu ambao ni lazima wacheze kama 'chale', huku nguo zao zikiwa kuukuu. Hii inaboa na kuzifanya sinema zetu kuzoeleka na kutabirika. Kiuhalisia jumba kubwa la mamilioni hawezi kukabidhiwa mtu kama huyo alilinde.

### Anarudi Ulaya na nguo ile ile

Hapa nadhani tatizo ni bajeti. Lakini inapoteza sana uhalisia. Mhusika anakwenda Ulaya. Halafu manonyeshwa anarejea anashuka Uwanja wa Ndege akiwa na nguo hiyo hiyo aliyokwenda nayo miaka mitano iliyopita. Tena siyo nguo tu, ila muonekano ni ule ule. Kiuhalisia haikupaswa kuchukua picha mhusika anasafiri na kurejea siku hiyo hiyo. Ilibidi wakae hata wiki. Abadilishe ngu na muonekano.

### Jini anasubiri magari, lazima acheke

Hapa kuna tatizo, waongozaji wangekuwa wanasubiri hakuna magari ndipo jini au mzimu uvuke. Badala yake wanafanya haraka, matokeo yake wanaanza kuangalia magari kabla ya kuvuka, hivyo kupoteza uhalisia. Kingine mtu yoyote ambaye ni katili au ambaye si wa kawaida, labda jini, mzimu akikutana na mtu ambaye anataka kumdhulu ni lazima acheke "Hahahahahahaha". Huku ni kukariri filamu zilizopita. Si lazima. Nadhani hii imeigwa kwenye video ya wimbo ya Michael Jackson, 'Thriller'.

### Gereza, kituo cha polisi vichekesho

Wakati wenzetu ukikuta mhusika yupo gerezaji au kituo cha polisi kuna uhalisia mtupu, tofauti na hapa kwetu.

Hii siwalaumu sana kutokana na jinsi tu sanaa yenyewe inavyochukuliwa Bongo. Kwa wenzetu wanaweza kuruhusiwa kuigizia kwenye kituo cha polisi mradi tu masharti yafuatwe. Pia kuna watu binafsi wanajenga vitu kama hivyo kwa ajili ya kukodisha kwa kampuni za waigizaji.

### Jambazi lazima avae koti refu



Kwa hali ya kawaida kabisa, mtu yoyote muovu huficha uhalisia wake wa moyoni. Kwenye filamu za Kibongo mtu yoyote muovu hasa jambazi ni lazima avae koti refu jeusi na mawani meusi. lengo siyo baya, kuweka uhalisia. Lakini si kila filamu mhusika anatakiwa ajulikane kuwa mtu mbaya hata kwa muonekano.

Wakati mwingine waovu hujificha si kwa kufanya wema na nguo tu, hata kuwa kwenye nyadhifa kwenye jamii.



# Cannon apata mtoto wa nane

MSANII wa filamu na mtangazaji wa TV, Nick Cannon, ametangaza ujio wa mtoto wake wa nane kutoka kwa mpenzi wake Bre Tiesi.

Hivi karibuni mwigizaji huyo maarufu alisema anatamani kuongeza idadi ya watoto wake, na Mungu akimpatia atapokea kwa furaha.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, amesema mtoto wake amezaliwa katika hali ya kawaida nyumbani jambo ambalo limempa uzoefu kuhusu uzazi.



## Kashfa ya kimapenzi yatikisa nyota Nigeria

SAKATA la mchungaji maarufu nchini Nigeria, Johnson Suleman, kijuhusisha kimapenzi na wasanii nyota wa filamu nchini humo linazidi kupamba moto.

Mtikisiko mkubwa umetokea baada ya mwandishi mmoja wa Blogu kutoa orodha ndefu ya mastaa wa kike wa filamu ambao alidai wamekuwa wakijihusisha kimapenzi na mchungaji huyo kwa nyakati tofauti.

Hata hivyo baadhi ya mastaa hao wamejitokeza kukana tuhuma hizo, huku mchungaji Sulemani moja ya jumbe zake kanisani kwake, ameeleza shutuma hizo kuwa sawa na kicheko.

“Nimesikia wananiburuza kwenye mitandao ya kijamii, huyo mtu ni shetani, shetani kakuua huko! Unataka kuniburuza? Aliuliza na kisha kusema ‘Tutajikokota,”.

## Bosi Mavin ampoteza mama yake

BOSI wa lebo ya muziki ya Mavin Records, Michael Collins Ajereh, maarufu kama Don Jazzy, ametangaza kumpoteza mama yake mzazi.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram wa lebo hiyo, Don Jazzy, amesema mama yake amefariki kutokana na ugonjwa wa saratani ambao ameugua muda mrefu.

“Nimempoteza mama yangu mpendwa, nguzo ya familia, msaidizi na ngao yangu,” ameandika.





## JLo, Affleck wala fungate Paris

WASANII maarufu nchini Marekani, Jennifer Lopez na Ben Affleck, wameamua kula fungate lao katika Jiji la Paris baada ya kufunga ndoa hivi karibuni.

Kulingana na mtandao wa PageSix, wanandoa hao walitua nchini Ufaransa siku ya Jumanne wakionekana wakiwa na mahaba mazito.


Jlo ambaye ni mkongwe katika muziki na Affeck anayetikisa katika filamu za Hollywood, walifunga ndoa ya siri na kisha walichagua Jiji hilo kuwa sehemu nzuri ya fungate yao.

## Rapa JayDa apigwa risasi

MWANAMUZIKI wa Hip hop kutoka Louisiana nchini Marekani, JayDa Youngan, yuko hospitali akiwa mahututi baada ya kupigwa risasi akiwa nyumbani kwake.

Polisi wa jimbo hilo walisema walipokea simu sita zote zikiripoti tukio hilo.

Aidha, walisema majeruhi huyo alikimbizwa hospitali ya karibu na mtu mmoja wa karibu na mtu mwingine ambaye pia alijeruhiwa katika tukio hilo na aliruhusiwa baada ya kupata matibabu.



MAKALA

# Ulaya, Russia inavyoiweka kati Afrika katika vita vya Ukraine

Na mwandishi Wetu


BARA la Afrika limegeuka kama uwanja wa mapambano kati ya mataifa ya Ulaya na Russia, katika juhudi za uungwaji mkono katika sakata la vita vinavyoendelea nchini Ukraine.

Kila upande unataka Nchi za Afrika ziwaunge mkono baada ya kuwapo kwa ukimya, huku baadhi zikiweka wazi kwamba hazina upande katika mgogoro huo.

Russia inatafuta kimbilio jipya kutokana na kutengwa na Nchi za Magharibi ambazo zimuiwekea vikwazo vya kiuchumi.

Hivi karibuni imeshuhudia zulia jekundu liliwekwa kwa ajili ya Waziri wa Mambo ya Nje Sergei Lavrov, wakati wa alipofanya ziara yake katika mataifa manne barani Afrika.

Ziara ya Lavrov ilionyesha jinsi Russia ingali na msuli wa kidiplomasia wa kuzipa changamoto Nchi za Magharibi kwa kuwa ndani ya mioyo na akili za serikali za Afrika, alipotembelea Misri, Ethiopia, Uganda na Congo-Brazzaville.



Rais wa Uganda Yoweri Museveni akimpokea Waziri wa Mambo ya Nje wa Russia, Sergey Lavrov wakati alipofanya ziara wiki iliyopita.

Mataifa mengi ya Kiafrika ikiwa ni pamoja na Nigeria na Kenya, Nchi zenye nguvu za kiuchumi za Afrika Magharibi na Afrika Mashariki zilipiga kura kuunga mkono azimio la mkutano mkuu wa Umoja wa Mataifa mwezi Machi, na kulaani uchokozi wa Russia na kutaka kujiondoa kutoka Ukraine.

Hata hivyo, nusu ya Nchi zote ikiwamo Tanzania hazikupiga kura kama kutoa jibu kwamba hazipo katika mfungamano wa upande wowote.

Afrika Kusini ambayo inahisi kuwa na deni kwa Russia kutokana na msaada wake katika vita dhidi ya utawala wa weupe walio wachache, huku Uganda inatazamiwa kushika uenyekiti wa vuguvugu la Nchi zisizofungamana na upande wowote, chombo kilichoundwa wakati wa Vita Baridi na Nchi ambazo zilitaka kukwepa kushikwa na ushindani kati ya madola ya Magharibi na kizuizi cha kikomunisti.

Katika mkutano na waandishi wa habari na Lavrov, Rais wa Uganda Yoweri Museveni alisisitiza msimamo wake wa kutoegemea upande wowote kuhusu mzozo wa Ukraine.

"Hatuamini kuwa maadui wa adui wa mtu," alisema.

Kwa upande wa Lavrov, ziara hiyo ilikuwa muhimu ili kupinga madai kwamba Nchi yake inasababisha njaa barani Afrika.

Alilaumu vikwazo vilivyowekewa dhidi ya Russia na mataifa ya Magharibi na kusababisha kupanda kwa bei ya nafaka.

Hakutoa msaada wowote kwa mataifa ya Afrika kukabiliana na athari za mzozo wa gharama ya maisha, lakini viongozi wa Afrika walimuelewa na kwa namna moja walimpa imani hawatamuangusha kutokana na Taifa hilo kuwaunga mkono wakati wa kupigania Uhuru.

Wakati Russia inateta na rafiki zake wa zamani, Ufaransa ikiungwa mkono na Ulaya iliamua kuzitembelea baadhi ya Nchi za Kiafrika kuweka ushawishi pamoja na kuipaka matope Russia, kuwa ndiyo mdudu anayetafuna ustawi wa bara hilo kwa kugeuza nafaka kama silaha.

Afrika inahitaji dola 1.3 ili kukabiliana na njaa au mpango wa Misheni ya Kustahimili Kilimo na Chakula (FARM) inayoongozwa na Ufaransa kusaidia kilimo cha Afrika.

Rais wa Ufaransa Emmanuelle Macron katika ziara yake ya Afrika wiki hii, akitembelea Cameroon, Benin na Guinea-Bissau, alishangazwa na kauli zinazosikika kuwa vikwazo vya Ulaya ndivyo vimeleta balaa la njaa .

"Tunalaumiwa na baadhi ya watu wanaosema kwamba vikwazo vya Ulaya ndiyo chanzo cha mzozo wa chakula duniani, ikiwa ni pamoja na Afrika. Ni uongo kabisa. Chakula, kama nishati, kimekuwa silaha za vita za Urusi." Alisistiza Macron

Akijibu kwa ukali maoni hayo, Lavrov alisema mzozo wa chakula ulianza tangu lilopoanza janga la Covid, lakini akakubali kwamba hali ya Ukraine iliathiri zaidi soko la chakula.

Akiwa Nchini Misri, Lavrov alitoa hakikisho kwamba wasafirishaji wa nafaka watatimiza ahadi zao.

Uchumi wa Misri unategemea zaidi Russia kuliko ule wa mataifa mengine mengi ya Afrika.

Takribani asilimia 80 ya uagizaji wake wa ngano hutoka Russia na Ukraine, na theluthi moja ya watalii wake wa kigeni ni Warusi.

Pia Nchi hiyo imeweka msingi wa kinu cha nyuklia cha dola bilioni 26 Nchini Misri.

Kijadi, biashara kati ya Russia na Afrika imezingatia ulinzi kutoka kwa uuzaji wa bunduki za moja kwa moja hadi ndege za kivita.

Hivi majuzi mamluki wa Russia wametumwa Mali na Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR) kusaidia vikosi vya serikali kutuliza uasi.

Katika ziara yake Lavrov pia aliangazia mkutano wa kilele kati ya Russia na Afrika unaotarajiwa kufanyika Nchini Ethiopia mwezi Oktoba, ambapo mikataba ya kibiashara na ulinzi inaweza kutiwa saini ili kuimarisha uhusiano.

Kwa upande wa Marekani mjumbe wake katika Pembe ya Afrika Michael Hammer, ambaye pia anazuru Misri na Ethiopia, wakati Balozi wake katika Umoja wa Mataifa, Linda Thomas-Greenfield, atakuwa Uganda na Ghana wiki ijayo.

Mataifa ya Magharibi yana nia ya kujionyesha yenyewe na pengine kuzikumbusha Nchi za Kiafrika kwamba inatoa zaidi katika njia ya biashara na misaada.



Rais wa Benin Patrice Talon akishikana mkono na Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron wakati alipofanya ziara nchini humo hivi karibuni.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAPOKWENDA...



# Kutoka kupora saa, cheni, hadi simu za 'tachi'

## ■Polisi nao waja na mbinu za kidigitali

Na Adam Fungamwango

ANISIKITISHA kijana Masudi, mambo yake, vitendo anavyovifanya mimi haviniridhishi. Masudi amekuwa kwapukwapu, mapesa mfukoni kachomoa, ukivaa saa nzuri kwapukwapu, vitambaa vya kichwani kwapukwapu, stendi ya basi ndiyo kwake..."

Huu ni wimbo unaoitwa 'Masudi' uliofyatuliwa mwanzoni mwa miaka ya 1980 katika bendi ya Dar International, utunzi wake Marijani Rajab.

Maana ya kuanza na wimbo huu ni kuonyesha kuwa thamani ya vitu huendana na wakati. Na hata, wahalifu, vibaka na wezi nao wanaiba au kupora vitu ambavyo kwa wakati huo vinakuwa kwenye chati. Nao pia wanakwenda na wakati.

Hebu fikiria wezi wa miaka 1980 walikuwa wanapora vitambaa vya kichwani wanavyovaa kinamama, saa, cheni, na hereni.

Baba akimwambia kijana wake kuwa zamani alishawahi kuporwa saa na vibaka, au kuchomolewa pesa mfukoni, atashangaa na wakati mwingine kucheka tu.

Mama akiwaambia wanaye kuwa alishawahi kuporwa kitambaa alichovaa kichwani, bangili, mkufu, au hereni, watashangaa. Ni vibaka gani hao ambao wanapora mitandio, ni vibaka kweli au?

Lengo la makala hii ni kuonyesha kuwa mageuzi, maendeleo, na hata kukua kwa teknolojia, hakufanyiki kwenye mambo mazuri tu, bali hata yale mabaya, hivyo kuwataka wananchi wawe makini na wasiishi kama walivyokuwa wakiishi zamani.

Ndiyo maana hata Jeshi la Polisi huwa linapeleka watu mafunzo kukabiliana na wahalifu ambao nao huwa wanabadilika kutokana na thamani ya vitu kwa wakati huo na teknolojia pia. Nalo pia si kama lile la zamani, bali ni la kisasa zaidi.

Jeshi la Polisi kwa sasa lina vitengo mbalimbali kama vya makosa ya kimtandao kutokana na wizi wa pesa kwa mitandao, wizi wa simu za kisasa, pamoja na uhalifu mwingine ambao ni wa kiteknolojia au kisasa zaidi.

Hii inaonyesha kuwa hata wahalifu nao huwa wanabadilika kutokana na nyakati.

Wakati Jeshi la Polisi likiwa limebadilika na kuwa na vitengo vya kidigitali kukabiliana na staili mbalimbali za uhalifu, wananchi nao wanapaswa kuwasaidia kwa kubadilika, kutoamini sana watu wasiowajua na kupenda biashara, kupata kazi au pesa ambazo zinaonekana zinapatikana kwa wepesi kuliko uhalisia.






Saa na mkufu, vitu ambavyo wezi zamani walikuwa wakiviwinda mno.

Tukirudi kwa wezi wa zamani, miaka ya 1980, vitambaa vya kichwani kwa kinamama ilikuwa ni kitu cha thamani sana. Nchi ilikuwa kidogo na matatizo ya nguo, kutokana na kumalizika kwa Vita ya Kagera, hivyo uchumi uliyumba kidogo.

Wezi walikuwa wakiwapora sana wakinamama vitambaa na kwenda kuviuza kwa akinamama wengine. Na waliwavizia wapo peke yao, au wakiwa wamekaa dirishani kwenye mabasi. Kibaka atanyata na kumpora, kabla ya kukimbia.

Hivyo hivyo ndivyo walivyofanya kwa akinamama waliokuwa waliokuwa amevaa hereni, bangili, mikufu au vyote kwa pamoja.

Vyote hivyo ni vitu ambavyo kwa wakati huo vilikuwa na thamani mno, kwani kibaka haikumchukua siku kupata wateja. Kwa sasa siyo hivyo tena, hakuna mwizi anayehangika navyo. Havina thamani tena.

Wezi au vibaka wa zamani, kwa asilimia kubwa walikuwa kwenye vituo vya basi. Mtu anaweza kutembea kote huko asiwe na wasiwasi, lakini akifika kwenye kituo cha basi, ni lazima awe makini sana, kwani walikuwa na uwezo mkubwa wa kuingiza mikono au vidole mfukoni bila mwenyewe kujua. Walitwa 'pick pocket.'

Walikuwa wanafanya kazi hiyo wakati wa abiria wanapogombea usafiri, au ndani ya basi. Ikumbukwe pia wakati huo kulikuwa na shida kubwa ya usafiri karibu jiji lote la Dar es Salaam.

Kwa sasa siyo hivyo tena. Wezi wapo sehemu zote na wala si kwenye vituo vya mabasi tu. Kwa sasa hawaingizi tena mikono mifukoni kama zamani, ila wanawaonea sana akinamama kwa kuchana na viwembe mikoba yao, na kuwachukuliwa simu, na pesa. Hii inawakumbusha akinamama kuwa makini sana, kwa sasa wakati wa kupanda daladala hasa kwenye vituo ambavyo usafiri ni wa shida, na hata wanapokuwa ndani ya gari wanapaswa mikoba yao kuweka mbele kifuani, au tumboni na si pembeni au mgongoni.

Kama nilivyosema miaka hiyo kulikuwa na uhaba wa nguo, hivyo wizi wa nguo pia ulikuwepo. Ukianika nguo nje na usipozilinda, basi imekula kwako.

Wezi wanaamua na kwenda kuuza. Kwa sasa wizi huo umepungua. Siyo kwamba wezi hawataki kuiba. Watamuuzia nani? Kwa sasa nguo za mitumba na nyingine zimekuwa nyingi, tena bei rahisi, si tu kwamba kila mmoja ana uwezo na kununua, lakini dunia ya sasa watu hawapendi kuvaliana nguo kwa sababu ya magonjwa.

Zilipoingia TV katikati ya miaka ya 1990, ambazo zilikuwa za 'chogo' wezi walikuwa wakizifuata mpaka ndani. Walivunja nyumba kwa kutumia jiwe maarufu lililoitwa 'Fatuma', wenyewe walikuwa wakiita 'kumi nje kumi ndani', yaani watu kumi waliingia ndani na wengine kubaki nje. Hao walifuata TV ya chogo tu. Kwa sasa hata ukimbebesha mtoto hata TV ya kisasa 'flat screen', umwambie apeleke kwa fundi, hawana hata mpango nazo. Ataenda nayo na kurudi bila kuguswa na mtu yoyote.

Hata watu wa kawaida mitaani walipoanza kumiliki simu za mkononi mwanzoni mwa miaka ya 2000, wizi na uporaji wa simu nao ukaingia. Simu yoyote ile iliporwa. Mradi ni simu. Lakini kadri teknolojia ilivyozidi kukua na kuwa na aina mbalimbali za simu, nao wakaanza kuchagua za kuiba au kupora.

Siku hizi simu za mkononi za kawaida maarufu 'viswaswadu' hata uiweke hapo, haibi mtu. Ukiisahau utaikuta na mwizi hana mpango nayo. Wizi na uporaji ukahamia kwenye simu janja, maarufu kama 'smartphone.'

Hali ilipozidi kuwa mbaya, watengenezaji wakabuni kutengeneza baadhi ya simu zenye 'GPS', teknolojia ya kitufe kinachokuwa ndani ya simu, mtu au kitu chochote lakini kinachoonyesha kilipo.

Jeshi la Polisi lina kitengo hicho na kimefanya kazi kubwa kuhakikisha wahalifu kukamatwa kiasi kwamba, wezi wameshaanza kuziogopa baadhi ya simu janja, maarufu kama za Tachi.'

Kwa siku za karibuni kumekuwa na wizi wa kutumia bodaboda na hasa akinadada wamekuwa waathirika sana.

Wanapaswa wawe makini wanapokuwa kando ya barabara na hasa wanapoziona bodaboda mbele yao, kwani wamekuwa wakiporwa mikoba yao, ambayo wanakuwa wameweka kila kitu ambacho walihitaji kukibeba. Wanawavamia, wanapora mkoba na kuondoka kwa kasi.

Wanapaswa kutoweka pesa, simu, vitambulisho na kila kitu kwenye sehemu moja yaani mkoba, lakini pia wawe makini kwenye kubeba mikoba yao kwa namna ambayo itakuwa vigumu kuporwa, au kutoonekana kirahisi, hasa nyakati za usiku.

**Tuma meseji 0716 350534**




Simu za mkononi 'smartphone', ni moja ya vitu ambavyo vibaka wa sasa wanavitolea macho.

## HABARI KIMATAIFA

# Russia yashambulia kila kona Ukraine

**KYIV,** UKRAINE

Jeshi la Russia limevishutumu vikosi vya Ukraine kwa kuua watu 40 baada ya kulishambulia gereza ambalo linawashikilia wafungwa wa vita wa nchi hiyo.

Tukio hilo lilitokea jana katika eneo linalodhibitiwa na waasi mashariki mwa Ukraine.

Wizara ya Ulinzi ya Russia katika taarifa yake imethibitisha kuuwawa kwa wafungwa 40 wa kivita wa Ukraine na kuwajeruhi wengine 75.

Taarifa hiyo ilieleza wafanyakazi wanane wa jela hiyo wamejeruhiwa katika shambulio hilo lilotokea eneo la Olenivka linalodhibitiwa na waasi wanaotaka kujitenga la Donetsk pia walijeruhiwa.

Huku haya yakijiri kwa mara ya kwanza baada ya wiki kadhaa, wanajeshi wa Russia wamefanya mashambulizi ya roketi kwenye mji mkuu wa Ukraine, Kyiv.

Kulingana na gavana wa mkoa wa Kyiv, Oleksiy Kuleba, watu 15 wamejeruhiwa katika mashambulizi hayo yaliyolenga vituo vya kijeshi kwenye viunga vya mji wa Kyiv.

Kuleba aliiambia televisheni ya taifa kwamba makombora zaidi pia yalianguka katika mji wa Chernihiv ulioko kaskazini mashariki mwa mji mkuu.

Mashambulizi pia yaliripotiwa katika mji wa Mykolaiv ambao uko karibu na mstari wa mbele wa kusini mwa nchi hiyo.

Mashambulizi hayo yalisababisha watu watano kuuawa katika kituo cha basi na kuwajeruhi wengine saba.

Ofisi ya rais wa Ukraine, Voloydmir Zelensky, jana ilisema kwamba makombora ya Russia yaliyoipiga Mykolaiv yaliharibu majengo kadhaa, pamoja na nyumba za makazi.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Antony Blinken alisema Russia imetoa vitisho vipya kwamba inatazamia kuchukua kimabavu maeneo zaidi ya Ukraine mbali na Donbas.

Aliongeza kuwa hatua kama hiyo haitahalalishwa kamwe.

Akizungumza na waandishi wa habari Blinken alisema "Nadhani ni muhimu sana sasa tuone nini mpango unaofuata wa Russia, huo ni unyakuzi wa eneo zaidi la Ukraine, Waziri wa Mambo ya Nje, Lavrov atasikia moja kwa moja kutoka kwangu kwa niaba ya Marekani, tunaona na tunajua wanachofanya na hatutakubali kamwe, haitahalalishwa kamwe, kutakuwa na matokeo ikiwa ndivyo wanavyofanya, na ikiwa ndivyo wanavyojaribu kudumisha"

Haya yanatokea wakati Marekani ilitangaza hapo juzi kuwa imewasilisha pendekezo kwa Russia la kuachiwa huru Wamarekani wawili wanaoshikiliwa nchini humo, akiwemo mchezaji maarufu wa mpira wa kikapu nchini Marekani, Brittney Griner.

Waziri wa Mambo ya kigeni wa Russia, Sergei Lavrov alisema nchi yake hivi karibuni itapendekeza siku ya mazungumzo hayo na Marekani.

**UKRAINE YAMTEUA MWENDESHA MASHTAKA**

Serikali ya Ukraine imemteua mwendesha mashtaka mpya wa serikali baada ya nafasi hiyo kuachwa wazi kwa karibu miaka miwili.

Mwendesha mashtaka huyo mpya Oleksandr Klymenko, ana umri wa miaka 35.

Hapo awali alifanya kazi kama mpelelezi katika idara ya taifa ya kupambana na rushwa.

Alipendekezwa kushika wadhifa huo tangu Desemba mwaka jana.

Ukraine inakabiliwa na shinikizo la kupambana na rushwa.

Kundi la nchi saba zilizoendelea kiviwanda zilipendekeza kuteuliwa kwa ofisa huyo wa kupambana na ufisadi baada ya mtangulizi wake Klymenko, Nazar Kholodnytsky, kujiuzulu Agosti mwaka 2020.

Mnamo mwaka jana, shirika la Transparency International liliikadiria Ukraine kama nchi ya pili miongoni mwa mataifa yanayoongoza kwa rushwa barani Ulaya

**DW**

# Maandamano yaisimamisha Guinea

**CONAKRY,** GUINEA

MAANDAMANO ya kuupinga utawala wa Guinea na ucheleweshwaji wa mchakato wa kurejesha demokrasia nchini humo, yamesababisha mji mkuu wa nchi hiyo, Conakry usimamishe shughuli nyingi.

Waandalizi wa maandamano hayo walidai kuwa mtu mmoja ameuawa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na mfungamano wa kitaifa wa ulinzi wa katiba (FNDC), mtu huyo aliuliwa kwa kupigwa risasi na watu wengine kadhaa wamejeruhiwa. Mfungamano huo wa kisiasa wenye ushawishi mkubwa nchini Guinea, uliandaa kampeni hiyo ya upinzani ili kushutumu uamuzi uliofanywa na utawala wa Guinea juu ya kuudhibiti mchakato wa kurejesha utawala wa kiraia, baada ya kutwaa madaraka mwaka uliopita.

Mwenyekiti wa jumuiya ya uchumi ya Afrika magharibi ECOWAS, Umaro Sissoco Embalom aliwataka watawala wa kijeshi nchini Guinea waharakishe hatua za kurejesha demokrasia **DW**





Ghasia zinazoambatana na uchomaji moto mali za Umoja wa Mataifa zinazidi kufanywa na Waandamanaji eneo la Goma nchini **DRC. PICHA: AFP**

# Kambi ya Umoja wa Mataifa yalipuliwa

**BENI,** DRC

KAMBI moja ya walinda amani wa Umoja wa Mataifa imelipuliwa kwa bomu la petroli huko Beni, mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Tukio hilo limetokea wakati kunaendelea maandamano yanayoambatana na ghasia kupinga uwepo wa umoja huo nchini DRC

Takribani vituo vingine viwili vya kulinda amani vilishambuliwa siku ya Alhamisi.

Takwimu za majeruhi hazikufahamika mara moja. Takriban watu 19 wakiwemo walinda amani watatu wa Umoja wa Mataifa wamefariki katika mapigano hayo makali kufuatia maandamano ya kupinga Umoja wa Mataifa yaliyoanza Jumatatu.

Waandamanaji wamekuwa wakishutumu Umoja wa Mataifa kwa kutowalinda raia dhidi ya makundi yenye silaha yanayoendesha shughuli zake mashariki mwa nchi.

Msemaji wa Umoja wa Mataifa alisema waandamanaji hao wameunganishwa na vikundi vya wanamgambo wa Mai Mai, vilivyoundwa kwa ajili ya kuwalinda wanakijiji.

Zaidi ya vikundi 100 tofauti vyenye silaha vinaendesha harakati zake mashariki, ikiwa ni pamoja na Allied Democratic Front ambayo inashirikiana na kundi la Islamic State.

Wimbi la hivi majuzi la mashambulizi limeua mamia na maelfu ya wengine kuyahama makazi yao.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## DEED POLL
**(On change of name)**
**(UNDER REGISTRATION OF DOCUMENT ACT)**
**Cap 117 R.E 2002**



**THIS DEED** is made this **24th day of July 2022.**
**BY THIS DEED**, the undersigned and the person with the name **KEZIA MAKUYA KITIKU OF P.O BOX 119 TABORA,** a citizen of the United Republic of Tanzania by birth Do **HEREBY ABSOLUTELY** renounce and abandon the use of my name **KEZIA JOSEPH KITIKU** which was mentioned in Citizen Identity Card **(NIDA)** with reference **No 19941211-43212-00003-12.**

**AND** in pursuance of such change of name as aforesaid I hereby declare that I shall at all times hereafter in all records, deeds and instruments in Writing and in all actions and proceedings and in all dealings and sign the name of **KEZIA MAKUYA KITIKU** as my name in lieu of the said names of **KEZIA JOSEPH KITIKU** renounced as aforesaid.

**THAT,** the reason for such change of name is due to adopts a full name of **KEZIA MAKUYA KITIKU** which was mentioned previously in Academic Certificates and birth Certificate **C No 1002800274**

**AND I HEREBY AUTHORISE** and request all person to designate and address me by such assumed name of **KEZIA MAKUYA KITIKU** only.

**IN WITNESS WHEREFORE,** I have hereunder signed my assumed named of **KEZIA MAKUYA KITIKU,** and have set my hand this **24th day of July, 2022.**

**SIGNED AND DELIVERED** by the said **KEZIA MAKUYA KITIKU.**
Who is known to me personally/identified TO me by **Rose RUZIGE**
The letter being known to me personally
This day of 27th July, 2022

K. Kitiku
**KEZIA MAKUYA KITIKU**

**BEFORE ME**
- Name: **CHRISTINA JACKSON**
- Qualification : **ADVOCATE**
- Signature:
- Date: 25th July 2025

## KUPOTEA KWA CHETI




**ALLY BAKARI ALLY** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye Index namba **S.2367/137** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **TOLEDO SEKONDARI mwaka 2015.** Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. **TAARIFA YA POLISI: DAR/URA/RB/299936/2022.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**VICTOR EMMANUEL MWEMEZI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.1599-0786** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari ya **BAOBAB** mwaka **2018**,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Polisi taarifa **KW/RB/3541/2022**

## KUPOTEA KWA VYETI



**YUSUPH KISEO NZOWA** anatangaza kupotelewa na vyeti,cha kidato cha nne chenye index namba **CS16000217537** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya **EAGLE SECONDARY** mwaka **2015**,na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **ACS19080193** kilichotolewa kupitia shule ya **ALPHA SECONDARY** mwaka **2019**, yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Polisi taarifa **DAR/CHU/RB/298218/2022**

## KUPOTEA KWA VYETI



**JOSEPH ELIAS MBOWE** anatangaza kupotea kwa cheti cha chuo cha **BACHELOR OF SCIENCE WITH COMPUTER SCIENCE** chenye usajili namba **23652/T.98** chenye namba **BSCWCOM 000008** kilichotolewa na **UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM mwaka 2001** na cheti cha chuo cha **MASTERS IN COMPUTER SCIENCE** chenye usajili namba **P 065/T.12** kilichotolewa na **UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM** mwaka 2007. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kwenye kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: UD/RB/3726/2016**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP JUDICIAL CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 130/2021**
**IN THE MATTER OF THE LATE**
**MARTIN KALIHOSE MWANDA......DECEASED**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR GRANT OF LETTERS OF ADMNISTRATION BY ABDUL ATHUMANI HIMBA.....PETITIONER**

**SUMMONS TO PRODUCE TESTAMENTARY PAPER**
**(section 60,rule 77)**

**To.GODWIN MARTIN KALIHOSE**

**WHEREAS** it appears to this court that a certain paper or witing being or reporting to be testamentary, to wit death, bearing date the 13th day of march 2020 of the late **MARTIN KALIHOSE MWANDA**,deceased,who died at lugalo hospital on the 13th of march 2020 is now in your possession or under your control.
**YOU ARE HEREBY COMMANDED** to produce,bring into and leave at this court the said paper or writing on or before 18th day of august 2022 after service hereof on you, inclusive of the day of such service.
This summons has been issued on the application of **ABDUL ATHUMANI HIMBA** of dar es salaam .
Given under my hand and the seal of the court,this 28 day of july 2022.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA KIHONDA**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......38/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: MWAMED JUMA NASSORO WA MAFISA KWA MAMBI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA MWANAIDI SHOMARY NASSORO**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 04 Mwezi 08 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 29mwezi 07 mwaka 2022**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MOROGORO MJINI**
**KITUO CHA KIHONDA, MKOA WA MOROGORO**
**SHAURI LA NDOA Na.40...2022**
**JINA LA MDAI: THABIT OMAR KITUPULA**
**JINA LA MDAIWA: SOPHIA ZUBERI ABDALLAH**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika Mahakama za Mwanzo)**

Kwa: **SOPHIA ZUBERI ABDALLAH ALIEPO TANGA - BARABARA YA 15**
Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba:Madai ya kwamba ndoa ivunjwe.Kwa hiyo unatakiwa Kuhuduria binafsi katika mahakama hii tarehe **03/08/2022** saa **09:30** asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:**Kama hautohudhulia siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitishwa kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,mahakama inaweza kusikiliza shauri hili bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 29/07/2022

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**MAHAKAMA YA WILAYA KINONDONI**
**SHAURI LA MADAI NO 36 YA 2022**
**EDINA WILLIAM KIMARIO.................. MDAI**
**DHIDI YA**
**ELIEZER MOSES KISIGILA.................. MDAIWA**
**JACKLINE ALPHONCE KATO.................MDAIWA**
**Kwa**
**ELIEZER MOSES KISIGILA NA**
**JACKLINE ALPHONCE KATO**
**JACKLINE ALPHONCE KATO NA ELIEZER MOSES KISIGILA**

**KUITWA SHAURINI**
Kwa kuwa mleta madai ameleta madai yake ambayo maelekezo yake yameelezwa katika nakala ya madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii. Kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria Mahakamani binafsi au wakili au muwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya tarehe 01 Mwezi wa agosti Mwaka **2022.**
Kwa mujibu wa madai haya na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutajwa shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

**ANGALIZO**
Kama hukuhudhuria siku tajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito wa kuitwa shaurini, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe **28 Mwezi Julai Mwaka 2022**

HAKIMU MKAZI
RESIDENT MAGISTRATE
KINONDONI DISTRICT COURT
DAR ES SALAAM

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie: 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani. Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa. Matokeo ya haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

# KAMA IPO, IPO TU-16

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

**MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani.**

**Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa.**

**Matokeo haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.**

****************************************

Kijiji cha Semwanza kilipokea ugeni. Watu wawili ambao hawakujulikana walipotoka, walifika kwenye ofisi za Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji.

Walionekana kuwa na sifa njema, na hawakuonekana kama wanatoka hata kwenye vijiji vya jirani, bali Mjini.

Walikuwa wamevaa nguo za gharama. Mmoja alikuwa mrefu mwembamba na mwenye nywele nyingi. Mwingine ni mfupi, mnene na alikuwa na kipara.

"Karibuni wageni." Ni sauti ya mwenyekiti ikiwakaribisha.

Wakaitikia kila mmoja kivyake na kuruhusiwa kukaa.

Baada ya makaribisho na maneno ya hapa na pale, mwenyekiti akaenda moja kwa moja kwenye mada.

"Enhee wageni wangu, kwanza mmetoka wapi na niwasaidie nini?"

Mrefu akajibu "Sisi tumetoka Chalinze mjini. Nia yetu ni kumuona kijana mmoja anaitwa Dibwela."


Mwenyekiti alishtuka kidogo. Jinsi walivyo na kumhitaji mwanakijiji wake Dibwela ilimshangaza.

"Vipi mnataka kukodisha shamba lake kulima?"

"Hapana, tuna mazungumzo naye." Akajibu tena yule yule.

"Kwa hiyo mnataka tumwite hapa ofisini tuzungumze naye, au mnataka kwenda nyumbani kwake."

"Nadhani nyumbani kwake ndiyo kuzuri zaidi." Akajibu mwingine.




**"Kwa hiyo mnataka tumwite hapa ofisini tuzungumze naye, au mnataka kwenda nyumbani kwake."**

"Okay, ngojeni nimwite kijana wangu awapeleke, mimi nina kikao hapa na watu fulani, wana matatizo ya mipaka ya shamba."

Dibwela alipokea ugeni ambao ulikuwa mgeni kabisa machoni mwake.

Huku nyuma hata Mwenyekiti wa Kijiji naye alikuwa na wasiwasi. Hakujua wageni wale wametoka wapi na nini walitaka kutoka kwa Dibwela.

"Dibwela, ugeni wako huu." Ilikuwa ni sauti ya kijana aliyetumwa na mwenyekiti kuwapeleka.

"Karibuni." Akawakaribisha kwa mashaka kidogo na mshangao kwa mbali. Akili ya haraka haraka ikamtuma kwamba huenda ni wanunuzi wa shamba.

"Nani aliyewaambia kuwa mimi nauza shamba?" Alijiuliza mwenyewe.

Aliingia ndani na kutoka na viti viwili vya marimba, akawapa kila mmoja na chake. Yeye akakaa kwenye kigoda.

Zikaja sekunde kadhaa za kusomana machoni. "Jamani mimi nawaacha, nimeshamaliza kazi yangu." Kijana akawashtua.

"We nenda, hawa wamefika." Dibwela akamjibu.

"Kijana, wewe ndiye Dibwela si ndiyo?"

Huku akiwa na wasiwasi kidogo, akajibu "Ndiyo mimi."

"Mimi naitwa Daudi." Yule mfupi ambaye ndiye alianzisha maongezi alijitambulisha, halafu akamtambulisha mwenzake mrefu mwembamba mwenye nywele nyingi.

"Huyu anaitwa Billy. Tumeelekezwa tuje kwako."

Hili liliendelea kumshangaza Dibwela na kujiuliza, watu wale wanaoonekana kama wametoka mbali, ni nani aliyewatuma, amewatuma nini na mtu gani huyo anayemfahamu hata kwa jina.

"Nani aliyewaelekeza na anataka nini?"

"Tumeambiwa wewe ndiye kaka yake msichana mmoja anaitwa Siwatu."

Mshituko mwingine ukampata. Awali alidhani huenda kuna kitu kibaya kwake, au watu hao walimlenga yeye, lakini hilo akaliondoa mara moja baada ya kusikia, anauliziwa dada yake.

"Kafanya nini tena, dada yangu, mbona kila siku mikosi." Akajibu kwa sauti kama mtu anayesikitika.

"Hakuna kibaya kwake bwana Dibwela." Billy akajibu.

"Kumbe?"

"Tumetumwa na bosi wetu, wanataka kumuoa."

Ni mshtuko juu ya mshtuko kwa Dibwela. Dada yake anataka kuolewa na mtu ambaye hamfahamu, amepata watu ambao hawafahamu pia.

"Ni nani, na anaishi wapi?"

"Anaishi Chalinze, yeye hana tatizo Siwatu, amesema kuna mtu amempa taarifa zake zote, hivyo anamfahamu kwa hiyo hana haja ya kumchunguza, sijui nini, ametupa barua hii ya posa, na amesema wewe ndiye ndugu yake pekee hapa."

"Anaitwa nani?"

"Sisi wafanyakazi wake tunamwita, Bosi Mulango, nadhani hilo ndiyo jina lale." Billy ndiye aliyeonekana kujibu maswali hayo magumu.

"Mmmh, haya, lakini juzi tu katoka kukataa barua ya mtu hapa kutoka kijiji cha jirani hapo na ni mkali kweli linapofika suala la kuolewa, sijui..." Dibwela akawa na wasiwasi, akikumbuka majuzi alipojibishana naye.

"Kaka sikiliza nikwambie. Kuolewa ni hiari ya mtu. Zile zama za kulazimishwa kuolewa zimepitwa. Mimi ukifika muda wa kuolewa nitaolewa. Na hata wewe hutokuja hapa kuniuliza, nitakuletea tu mtu, au mshenga atakuja kwako. Kama Mungu amepanga mimi niolewe, au siku moja niondokane na hii mikosi inayonipata sawa, ila sitoishi kwa kuangalia nani anasemaje.

Kaka nikwambie, hakuna umri wa kuolewa. Ila kuna utayari wa kuolewa. Tena kuolewa na mtu ambaye umeridhika naye kaka."

Akawa anakumbuka maneno ambayo alikuwa akiongea Siwatu, wakati akipinga kuolewa kwa mara ya pili, kwanza ilikuwa ni Maiko ambaye ndiyo ilisemakana kwa hasira akambaka, ingawa hakukuwa na ushahidi wa moja kwa moja, bali kukutwa kwa leso yake chumbani kwa Siwatu, siku kadhaa baada ya tukio hilo.

"Sasa sijui twende kwake au..."Wakati akiongea hivyo alipita mtoto mmoja wa kike. "We Mwaka, unaenda huko, pitia kwa Siwatu, ukimkuta mwite, mwambie aje hapa kuna wageni wake, aje haraka sana." Dibwela alimtuma na mtoto akaitikia kwa kichwa.

"Unajua, mimi nataka sana dada yangu aolewe, amepata tabu sana hapa kwenye hiki kijiji, tena kama akitoka hapa na kwenda kwingine itakuwa vizuri sana, ila sijui anakwenda wapi na huyo mwanaume ni nani na atamtunza vipi." Dibwela alieleza wasiwasi wake.

"Usiwe na wasiwasi kaka, kama dada yako akikubali, utamuona huyo shemeji yako, siyo mtu mbaya, tumekwambia anaishi Chalinze, ni bosi wetu. Siyo kwamba ana pesa sana, hapana, ila kama uwezo wa kumtunza dada yako anao sana tu." Daudi akamtoa wasiwasi.

"Tungeweza kuja naye, lakini si unajua mila tena za Kiafrika, tumeleta barua, tuje na mhusika, hapana. Sisi tumeelekezwa tuje hapa kama washenga, nyinyi ndiyo mtapanga siku ya yeye kuja kujitambulisha." Akadakia Billy.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# COASTAL YANOGEWA NA NYOTA WA ZENJI

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Coastal imesajili wachezaji wanne kutoka Zanzibar katika kile kinachoonekana kukiimarisha kikosi chao kwa msimu ujao wa Ligi Kuu na mashindano mengine.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Juma Mgunda amesema wameanza kukiimarisha kikosi hicho, na anaamini kitakuwa bora zaidi msimu ujao kuliko uliopita.

Coastal imeonekana safari hii kukimbilia zaidi kusajili wachezaji kutoka Ligi Kuu ya Zanzibar kama Maabad Maulind Maabad ambaye ni mshindi wa kiatu cha dhahabu kwenye ligi hiyo, akitokea klabu ya KVZ, winga Msati Kassim 'Gabo' kutoka Malindi, beki Idarous Seif 'Yobo' kutoka Jang'ombe na Khatib Kombo 'Hero' kutoka Kipanga.

**Mbali na wachezaji kutoka Zanzibar, Coastal pia imewasajili wachezaji wa kigeni Mkongomani Riquene Pembele, ambaye anacheza nafasi ya winga, kiungo Djibril Olatoundji raia wa Benin na kipa Mamahoud Mroivili kutoka Comoro.**

Mgunda amesema anafurahia usajili huku akipata fursa ya kuiandaa timu mwenyewe, tofauti na msimu uliopita ambapo aliichukua kwenye hali mbaya.

"Sisi makocha wakati mwingine unakuwa kama unajitoa mhanga, inatakiwa uwe na roho ngumu, kwa sababu unapewa timu ikiwa kwenye hali mbaya, lakini unakubali unafanya kila njia ili kuinusuru. Ndivyo nilivyofanya mimi msimu uliopita, lakini safari hii nafurahi kwa sababu nauona usajili na nitaanza kuiandaa mwenyewe timu ya msimu ujao," alisema straika huyo wa zamani wa timu hiyo na timu ya taifa, Taifa Stars.

Coastal imeondokewa na wachezaji wake kadhaa muhimu, wakiwemo Victor Akpan aliyekwenda Simba, Abdul Selemani 'Sopu' aliyetwaliwa na Azam FC, Rashid Chambo na Muhsin Makame waliosajiliwa na Dodoma Jiji.



Ally Choki na Luiza Mbutu wakifanya vitu vyao

# Pwani Sensa Soka Bonanza yaja

Na Sabato Kasika, KIBAHA

TIMU 14 za soka kutoka kata 28 za Kibaha Mjini na Vijijini mkoani Pwani, zinatarajiwa kuchuana katika Bonanza lilitwalo Pwani Sensa Soka Bonanza likiwa na lengo la kuhamasisha watu kujiandaa kuhesabiwa katika sensa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi wa Linda Media Solution (LIMSO) Khadija Kalili, alisema bonanza hilo litafanyika Agosti 14, na limeshapata baraka za Ofisa wa Michezo wa Mkoa, Grace Bureta.

"Timu ambazo zitaibuka na ushindi kuanzia wa kwanza hadi wa tatu, zitaondoka na zawadi tutakazozitangaza hapo baadaye, kwani kwa sasa tunaendelea na maandalizi ya michuano hiyo," alisema Kalili.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa kabla ya michuano, kutakuwa na burudani ya muziki kutoka kwa vikundi vya wasanii mbalimbali, kwa ajili ya hamasa kusaidia kufanikisha lengo la kuhimiza watu kujiandaa kuhesabiwa.

Alisema, kutakuwa na mechi ambazo zitakutanisha timu mbalimbali ndani ya wilaya ya Kibaha, ambapo ametoa wito kwa wadau wa soka kujitokeza kusaidia bonanza hilo, kwa kuwa sensa ni muhimu.

Alifafanua kuwa Ofisa Michezo mkoa huo amewapongeza kwa kuleta wazo hilo la kufanya bonanza, kwa ajili ya kuhamasisha watu kujiandaa kuhesabiwa katika sensa, kwamba ni zuri na lina tija kwa taifa.

"Linda Media Solution kwa kushirikiana na vyama vya soka Mkoa wa Pwani imeandaa bonanza hili la mpira wa miguu, litafanyika kwenye viwanja vya Bwawani vilivyopo Mailimoja wilayani Kibaha mkoani Pwani," alisema.

Alisema, ni wajibu wa kila Mtanzania kutoa hamasa ili kufanikisha sensa ambayo inatarajiwa kufanyika Agosti 23 mwaka huu, ambapo amewaomba wadau mbalimbali kujitoleza kuwaunga mkono.

# Twanga kupeleka mpya Tabora, Mpanda

Na Sabato Kasika

BENDI ya muziki wa dansi ya Twanga Pepeta, inatarajia kutambulisha nyimbo mpya zinazoandaliwa kwa ajili ya albamu ya kwanza ya mwaka 2022 katika miji ya Tabora na Mpanda wakati wa sikukuu ya Nanenane.

Mwimbaji nyota wa bendi hiyo Ally Choki, alisema Twanga ataelekea mkoani Tabora kuanzia Agosti 3 mwaka huu na kisha itafika Mpanda mkoani Katavi kwa ajili ya kuendelea kutoa burudani huko.

"Kwa sasa tuna nyimbo mpya zikiwamo za Chombo ya Fundi, Dokta Ruby utunzi wangu, Mbea utunzi wa Khalid Chokoraa na Shobo wa mwimbaji chipukizi Joshua tutazitambulisha katika ziara hiyo," alisema Choki.

Mbali na kuzungumzia ziara hiyo, Choki alisema bendi hiyo inajiandaa kuweka mikakati ya kuhakikisha muziki wa dansi unabaki kwenye mstari baada ya kukumbana na changamoto nyingi.

Choki alisema miongoni mwa mikakati hiyo ni kuendelea kuandaa nyimbo ambazo zinakuwa na mvuto kwa mashabiki na hata kuandaa maonyesho ya kuwapa nafasi ya kutoa maoni baada ya kusikiliza nyimbo mpya.

Alisema, kila bendi ina mikakati yake ya kuhakikisha inaendelea kusimama imara, na kwamba kwa upande wa Twanga, hiyo ni baadhi ya mikakati wanayotarajia kuitumia ili kuendelea kusimama imara.

"Siyo siri kwamba muziki wa dansi unapitia changamoto nyingi na kusababisha baadhi ya bendi kuyumba, lakini ninaamini kuwa bado upo kwenye mstari, hivyo kuhakikisha unaendelea kuwa na nguvu," alisema.

Alisema bendi imeweza kukabiliana na yote na bado iko imara, na kwamba zaidi ya mwongo mmoja imeendelea kuwatumbuiza mashabiki wake ndani ya changamoto zinazoukabili muziki wa dansi.

## ZISIKUPITE

### GUEYE AWANIWA EVERTON

KLABU ya Everton imewasiliana na Paris St-Germain kuhusu kumsajili tena kiungo wa kati wa Senegal, Idrissa Gueye mwenye umri wa miaka 32, huku mazungumzo yakiendelea siku chache zijazo. (***Fabrizio Romano***)

### TAVARES ATUA MAESEILLE

NUNO Tavares mwenye umri wa miaka 22 jana Ijumaa alifanyiwa vipimo vya afya na Marseille baada ya timu hiyo ya Ufaransa kukubaliana kumchukua kwa mkopo kutoka Arsenal. (***Fabrizio Romano***).

### SANCHEZ ATAKIWA

KLABU ya Marseille pia imeanza mazungumzo ya kumsajili mshambuliaji wa Chile, Alexis Sanchez mwenye umri wa miaka 33 kutoka Inter Milan. (***L'Equipe***)

### KOSTIC AWANIWA

KLABU ya West Ham inaendelea na mazungumzo na Eintracht Frankfurt kuhusu kumsajili mchezaji wao wa kimataifa wa Serbia, Filip Kostic mwenye umri wa miaka 29, ambaye anaweza kucheza kama beki wa kushoto au winga wa kushoto. (***90min***)

### ZANIOLO AWINDWA

KLABU ya Tottenham itajaribu kuipiku Juventus katika uhamisho wa fowadi wa Italia, Nicolo Zaniolo mwenye umri wa miaka 23 kutoka Roma. (***Tuttosport***)

### REGUILON AWANIWA BARCA

BARCELONA wana nia ya kumsajili Sergio Reguilon mwenye umri wa miaka 25 kutoka Tottenham Hotspur, ikiwa hawataweza kumsajili beki wa kushoto wa Hispania, Marcos Alonso mwenye umri wa miaka 31 kutoka Chelsea. (***AS***)

### KETELAERE KUTUA MILAN

AC Milan wamekubali mkataba wa kumsajili Charles de Ketelaere kutoka Club Bruges, licha ya Leeds United na Leicester City kumtaka mshambuliaji huyo wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 21. (***90min***)

### GIOVANI AKATALIWA

KLABU ya Palmeiras imekataa ofa mbili kutoka kwa Ajax kwa ajili ya kumsajili mshambuliaji wa Brazil, Giovani mwenye umri wa miaka 18 na timu hiyo ya Uholanzi sasa inakabiliwa na ushindani mkali kutoka kwa Newcastle na Bayer Leverkusen. (***ESPN***)

### TRIPPIER NUSURA ATUE MAN

MLINZI wa pembeni wa Newcastle United na England, Kieran Trippier mwenye umri wa miaka 31 amesema angeweza kujiunga na Manchester United msimu uliopita wa joto, kabla ya kuamua kuondoka Atletico Madrid na kujiunga na Newcastle, Januari. (***Mirror***)

### LOOKMAN KUUZWA

KLABU ya Everton inatazamiwa kupokea ada ya kumuuza Ademola Lookman huku Atlanta ikikubali kumsajili winga huyo wa Nigeria mwenye umri wa miaka 24 kutoka RB Leipzig kwa ada ya euro milioni 15. (***Sky Sport Italia***)

### FIRMINO KUTOONDOKA

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amepuuza mapendekezo ya mshambuliaji wa Brazil, Roberto Firmino kuondoka msimu huu wa joto baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 kuhusishwa na Juventus na Newcastle. (***90min***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO AJIBU KUHUSU HATIMA YAKE MAN UTD

## Asema anazushiwa uongo mwingi, awacheka mashabiki wa Atletico Madrid...

**MANCHESTER,** England

CRISTIANO Ronaldo ametumia mitandao ya kijamii kukemea 'uongo' unaohusu mustakabali wake ndani ya Manchester United.

Ronaldo ameomba kuondoka Old Trafford msimu huu wa joto huku pia akikosa nafasi ya kuwepo kwenye kikosi cha mandalizi ya msimu mpya kwa sababu ya matatizo ya kifamilia.

Akijibu ujumbe kupitia Instagram unaodai kuwa Sir Alex Ferguson alishiriki katika mkutano wa hivi karibuni na kumzuia Ronaldo kuondoka - alisema 'uongo' mwingi unazunguka kuhusu mustakabali wake.

"Haiwezekani kutozungumza kunihusu kila siku," aliandika.

**Ronaldo pia alichukua sehemu ya maoni ya chapisho lingine kuhusu maandamano yanayoendelea kutoka kwa mashabiki wa Atletico Madrid dhidi ya uwezekano wa uhamisho wake.**

Hivi majuzi baadhi ya mashabiki waliinua bango lililosomeka 'Ronaldo haukaribishwi'.

United wameweka wazi kwa Ronaldo kwamba hawataki kumuuza msimu huu wa joto, huku kocha mpya Erik ten Hag akikiri wazi kuwa anataka mshambuliaji huyo mkongwe awe sehemu ya kikosi chake kwa ajili ya msimu huu.

Hata hivyo, Ronaldo anataka kujiunga na klabu iliyopo kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya.

Atletico na Bayern Munich zote zimehusishwa lakini zimekanusha uvumi huo hadharani, huku Chelsea pia wakikataa kumuwania.

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,018,1


MECHI KALI
LIVERPOOL
VERSUS
MANCHESTER CITY
1 | 2.65
X | 3.23
2 | 2.43

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ALISSON, JOTA KUWAKOSA MAN CITY LEO



**LONDON,** England

NYOTA wa Liverpool, Alisson na Diogo Jota wameondolewa kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Manchester City leo kwa sababu ya kuwa majaeurhi.

Alisson hajahusika tangu mechi ya kirafiki ya kujiandaa na msimu mpya dhidi ya Manchester United mjini Bangkok Julai 12.

Mlinda mlango huyo wa Brazil sasa ameanza mazoezi tena lakini hatakuwa tayari kukabiliana na City katika mechi ya kufungua pazia la msimu huu katika Uwanja wa King Power.

Hata hivyo, kocha Jurgen Klopp abakiwa na amatumaini kuwa mlinda mlango wake atakuwepo kumenyana na Fulham wakati Liverpool itafungua Ligi Kuu ya msimu wa 2022/23 dhidi ya Fulham, Agosti 6.

Jota, kwa sasa anauguza jeraha la misuli na haijafahamika ni lini atarejea.

"Alisson na Diogo hawatakuwepo (dhidi ya Man City)," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari Alhamisi.

"Ali amefanya mazoezi leo (juzi) zaidi ya siku iliyopita kwa hiyo atapatikana kwa Fulham, lakini sio hii wikendi.

"Hivyo hivyo kwa Diogo. Diogo hakuwepo nasi kwa hiyo angewezaje kucheza mchezo wa soka? Hiyo itachukua muda kwa bahati mbaya. Ni hivyo."


Kipa chaguo la tatu wa Liverpool, Adrian anatarajiwa golini kwenye mchezo huo.

Mhispania huyo alikuwa nyuma ya Caoimhin Kelleher katika mechi ya Anfield, lakini raia huyo wa Ireland anaungana na Alisson kutopatikana kwa mechi ya Jumamosi.

Mchezaji aliyesajiliwa majira ya kiangazi Darwin Nunez yuko mbioni kucheza mechi yake ya kwanza rasmi Liverpool.

Mchezaji huyo wa Uruguay, ambaye uhamisho wake kutoka Benfica iligharimu kiasi cha pauni milioni 85, alifunga mara nne katika mechi za maandalizi ya msimu mpya.

# Kounde afichua sababu kuitosa Chelse



**BARCELONA,** Hispania

JULES Kounde amekiri kwamba, kocha wa Barcelona, Xavi alikuwa na mchango mkubwa katika uamuzi wake wa kuchagua, kujiunga na timu hiyo badala ya Chelsea.

Chelsea walikuwa na makubaliano kamili na Kounde na Sevilla mapema mwezi huu lakini beki huyo wa kati alichelewesha uamuzi wa mwisho na kuipa Barcelona muda wa kufikia ofa ya The Blues, na hatimaye kukubali kuhamia Camp Nou mara tu klabu hizo zilipofikia makubaliano.

Huku uhamisho wake sasa ukiwa haujakamilika, Kounde alizungumza na Barca TV kumpongeza Xavi kwa jukumu lake katika kuhitimisha sakata hilo.

"Xavi anawajibika kwa kiasi kikubwa (kwa uamuzi)," alisema Kounde. "Maongezi yake yalinisisimua.

"Nilizungumza naye mara kadhaa. Mazungumzo yalikuwa magumu sana
alinipa hisia kwamba, tunaona soka kw
njia sawa. Nitakuja pia natumaini nitafa
ya kila niwezalo kucheza nafasi ya uongo
kwa klabu hii."

Beki huyo aliongeza: "Najivunia san
nashukuru na nimefurahi kwa sabab
nimefika katika klabu kubwa sana yen
timu ambayo iko hivyo, nataka kuanza k
cheza na timu na kujiunga na wenzang
haraka iwezekanavyo. .

"Sevilla ni klabu kubwa lakini Barcelon
ni hatua moja zaidi katika maisha yang
katika kila ngazi, hasa michezo. Nitajarib
kushinda mataji mengi iwezekanavyo."

Kounde anajiunga na safu ya ulinzi
Barcelona ambayo tayari imemuonge
Andreas Christensen kutoka Chelse
huku Xavi sasa akijivunia safu ya beki w
kati ambao pia wanamjumuisha Rona
Araujo, Gerard Pique na Eric Garcia.

## HABARI MICHEZO


16,895/-

SUPA JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 30/07/22 | 17:00 | Cardiff vs Norwich City | 3.09 | 3.29 | 2.29 |
| 02. 30/07/22 | 17:00 | Millwall vs Stoke City | 2.26 | 3.34 | 3.09 |
| 03. 30/07/22 | 17:00 | Rotherham vs Swansea | 2.94 | 3.43 | 2.31 |
| 04. 30/07/22 | 17:00 | Wigan vs Preston | 2.40 | 3.19 | 2.99 |
| 05. 30/07/22 | 17:00 | Bristol Rovers vs Forest Green | 2.33 | 3.33 | 2.98 |
| 06. 30/07/22 | 17:00 | Carlisle vs Crawley Town | 2.27 | 3.28 | 3.13 |
| 07. 30/07/22 | 17:00 | Kilmarnock vs Dundee Utd | 2.26 | 3.24 | 3.19 |
| 08. 30/07/22 | 17:00 | St. Johnstone vs Hibernian | 2.98 | 3.08 | 2.47 |
| 09. 30/07/22 | 17:00 | Morecambe vs Shrewsbury | 2.94 | 3.29 | 2.38 |
| 10. 30/07/22 | 18:30 | GIF Sundsvall vs Varbergs Bois | 2.70 | 3.40 | 2.50 |
| 11. 30/07/22 | 19:00 | Odd Ballklubb vs Rosenborg | 3.03 | 3.38 | 2.28 |
| 12. 30/07/22 | 19:00 | Liverpool vs Manchester City | 2.62 | 3.18 | 2.45 |
| 13. 30/07/22 | 19:15 | Oostende vs Mechelen | 2.70 | 3.45 | 2.48 |
| 14. 30/07/22 | 19:30 | Enppi Club vs Al Masry Club | 3.02 | 2.98 | 2.48 |
| 15. 30/07/22 | 20:00 | Nimes vs Caen | 2.71 | 3.22 | 2.66 |
| 16. 30/07/22 | 20:00 | Le Havre vs Grenoble Foot | 2.33 | 3.08 | 3.33 |
| 17. 30/07/22 | 20:00 | US Quevilly Rouen vs Rodez Aveyron | 2.62 | 3.07 | 2.87 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 30/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1542 | Jeonbuk Hyundai vs Jeju Utd | 1.90 | 3.49 | 3.49 |
| 13:00 | 3516 | Gamba Osaka vs Kyoto Sanga | 2.39 | 3.14 | 2.75 |
| 13:00 | 3712 | Urawa Red Diamonds vs Kawasaki Frontale | 2.60 | 3.24 | 2.46 |
| 13:00 | 5896 | Ulsan Hyundai vs Gangwon | 1.53 | 3.86 | 5.28 |
| 14:00 | 5944 | Livingston vs Rangers | 7.63 | 4.62 | 1.37 |
| 14:30 | 1973 | Arsenal vs Sevilla FC | 1.80 | 3.58 | 3.77 |
| 14:45 | 1133 | Manchester Utd vs Atletico Madrid | 2.12 | 3.33 | 3.05 |
| 16:00 | 1577 | Degerfors vs Kalmar | 3.82 | 3.43 | 1.83 |
| 16:00 | 4724 | Dijon vs St Etienne | 2.85 | 3.10 | 2.46 |
| 16:30 | 1881 | Jahn Regensburg vs FC Koln | 5.71 | 4.59 | 1.50 |
| 16:30 | 2493 | Bayreuth vs Hamburger SV | 8.32 | 5.89 | 1.30 |
| 16:30 | 2530 | SV Elversberg vs Bayer Leverkusen | 12.28 | 6.96 | 1.20 |
| 16:30 | 2941 | Illertissen vs Heidenheim | 12.20 | 6.31 | 1.22 |
| 17:00 | 1252 | Cardiff vs Norwich City | 2.95 | 3.20 | 2.34 |
| 17:00 | 2471 | Millwall vs Stoke City | 2.27 | 3.15 | 3.10 |
| 17:00 | 2626 | Blackburn vs QPR | 2.01 | 3.40 | 3.45 |
| 17:00 | 2646 | Blackpool vs Reading | 1.99 | 3.39 | 3.54 |
| 17:00 | 2836 | Rotherham vs Swansea | 2.61 | 3.36 | 2.51 |
| 17:00 | 3106 | Luton Town vs Birmingham | 1.86 | 3.44 | 3.99 |
| 17:00 | 3737 | Kilmarnock vs Dundee Utd | 2.40 | 3.11 | 2.96 |
| 17:00 | 3982 | Wigan vs Preston | 2.45 | 3.10 | 2.85 |
| 17:00 | 4471 | Zlin vs Mlada Boleslav | 2.90 | 3.35 | 2.40 |
| 17:00 | 4931 | Hull City vs Bristol City | 2.33 | 3.21 | 2.96 |
| 17:00 | 5013 | St Johnstone vs Hibernian | 3.21 | 3.01 | 2.32 |
| 17:00 | 5537 | Hearts vs Ross County | 1.54 | 4.03 | 5.64 |
| 17:00 | 5758 | Cercle Brugge vs Anderlecht | 3.47 | 3.42 | 2.02 |
| 17:00 | 5966 | Honka vs VPS Vaasa | 1.56 | 3.92 | 4.90 |
| 17:30 | 4076 | Zenit St Petersburg vs Lokomotiv Moscow | 1.29 | 5.41 | 8.22 |
| 18:00 | 1092 | Dinamo Brest vs Vitebsk | 2.46 | 3.10 | 2.70 |
| 19:00 | 2753 | Liverpool vs Manchester City | 2.65 | 3.23 | 2.43 |
| 19:00 | 3463 | Stuttgarter Kickers vs Greuther Furth | 16.28 | 7.33 | 1.16 |
| 19:00 | 3751 | Odd Ballklubb vs Rosenborg | 3.02 | 3.37 | 2.24 |
| 19:00 | 4508 | Carl Zeiss Jena vs VfL Wolfsburg | 21.39 | 9.58 | 1.10 |
| 19:00 | 4570 | Tromso vs Sandefjord | 1.48 | 4.32 | 6.03 |
| 19:00 | 4933 | Kickers Offenbach vs Fortuna Dusseldorf | 6.12 | 4.28 | 1.51 |
| 19:00 | 5974 | Ham-Kam vs Kristiansund | 1.83 | 3.67 | 3.92 |
| 19:15 | 3048 | Oostende vs Mechelen | 2.67 | 3.42 | 2.45 |
| 19:15 | 3773 | OH Leuven vs KVC Westerlo | 2.33 | 3.37 | 2.87 |
| 19:30 | 1401 | Middlesbrough vs West Bromwich | 2.17 | 3.30 | 3.15 |
| 20:00 | 1927 | Teplice vs Viktoria Plzen | 6.31 | 4.48 | 1.47 |
| 20:00 | 2553 | Sochi vs Akhmat Grozny | 2.05 | 3.45 | 3.30 |
| 20:30 | 5872 | Sturm Graz vs RB Salzburg | 4.42 | 3.83 | 1.63 |
| 20:45 | 1156 | Trabzonspor vs Sivasspor | 1.79 | 3.34 | 4.11 |
| 21:00 | 5884 | Ajax vs PSV Eindhoven | 1.78 | 3.68 | 3.77 |
| 21:30 | 2060 | RB Leipzig vs Bayern Munchen | 3.39 | 3.79 | 1.85 |
| 21:30 | 4569 | FC Sion vs Servette Geneva | 2.51 | 3.51 | 2.56 |
| 21:45 | 1223 | KAA Gent vs St Truiden | 1.56 | 3.98 | 5.44 |
| 22:00 | 3022 | Arab Contractors vs Al Ahly Cairo | 6.00 | 3.85 | 1.54 |
| 22:00 | 3628 | Minnesota Utd vs Portland Timbers | 1.83 | 3.82 | 3.97 |
| 22:45 | 5549 | Porto vs Tondela | 1.11 | 7.07 | 17.66 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# BONDIA KIDUNDA AAHIDI KUMDUNDA KATOMPA LEO

**Na Saada Akida**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Selemani Kidunda ameahidi ushindi wakati atakapozichapa na Tshimanga Katompa kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), pambano linalofanyika leo katika uwanja wa majimaji, Songea.

Kidunda amedhamiria kufanya kweli katika pambano hili la kuwania mkanda wa ubingwa wa Dunia wa WBF.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kidunda alisema amejipanga vizuri na kwamba, atatoa kipigo cha nguvu kwa mpinzani wake huyo.

Alisema amefanya maandalizi mazuri kwa ajili ya kuhakikisha anamchapa mpinzani wake huyo kwa kulipa kisasi baada ya Katompa kumpiga faulo mbaya na kufanya pambano hilo la mwaka jana kuahirishwa na kurudiana leo.

"Wakongo ndiyo zao kuongea, msiwe na wasiwasi, nitampiga huyu, mimi nimefanya mazoezi na kazi yangu nitaonyesha kesho (leo) ulingoni kwa kumchapa, baada ya awali kumkosa kwa pambano kuahirishwa kutokana na faulo mbaya," alisema Kidunda.

Naye Katompa alitamba kwamba, amejiandaa kumpiga Kidunda nyumbani kwake na kuondoka na mkanda huo.

Alisema yuko tayari kwa pambano hilo kwa kuwa Kidunda wanamchukulia kama bondia mchanga kwenye mchezo huo kwa kutumia neno baby hivyo hatoweza kuwasumbua.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Athuman Nyamlani akiwa kwenye picha ya pamoja na washiriki wa kozi ya Ukocha ya CAF C Diploma iliyofanyika Makao Makuu ya TFF, Karume, Ilala, jana. **PICHA: TFF**

# Maji yanacheza muziki Dubai

**Na Sabato Kasika**

WATU wanaotamani kutembelea Dubai, wamekumbushwa kuwa kuna vivutio vingi tofauti kikiwamo cha jinsi maji yanavyoweza kucheza muziki wa wasanii tofauti duniani na vivutio vingine vingi.

Mkurugenzi wa Rivexcel Tonye Princewill, ambayo ni kampuni ya kutangaza utalii wa Dubai, aliliambia gazeti hili jijini Dar es Salaam jana kuwa ni muhimu kwa mtu kwenda nchini humo kujua jinsi ilivyopiga hatua.

"Baadhi ya vivutio hivyo ni Palm Fountain Jumeirah, sehemu unayoweza kutazama maji yakicheza. Kuna njia mbili juu na chini na taa za LED 3000 zinazomulika maji hayo yanaporuka juu kupitia njia zake," alisema Princewill.

Alifafanua kuwa maji hayo yanaruka na kucheza muziki wa wasanii tofauti duniani na kwamba shoo hiyo huwa inaanza baada ya jua kuzama hadi usiku, na kwamba ni kivutio cha pekee.

"Lakini pia Alserkal Avenue, kwa ajili ya mashabiki wa magari ambapo wanaweza kuona magari ya kila aina duniani kuanzia BMW, Ferrari, Porsche, magari haya ni ya viwango vya juu," alisema.

Alisema watu watashangazwa kuona jinsi jangwa lililotengenezwa kuwa mji ambao ni kivutio kikubwa duniani na nyumba ya teknolojia. Makumbusho haya yanapatikana maeneo ya Deira pale Souk Al Marfa.

Mkurugenzi huyo alitaja pia Museum of the Future ambayo ipo Barabara ya Sheikh Zayeed, ambapo ndani ya jengo hilo kuna teknolojia za kila aina zilizotengenezwa na wahandisi wa Dubai.

"Vilevile kuna Dubai Aquarium and Underwater zoo ambalo ni bwawa kubwa la samaki wa kila aina wapatikanao duniani, lakini pia kuingia Dubai Mall ni bure kabisa," alisema.

Michezo
Nipashe
Jumamosi Julai 30, 2022



Ronaldo ajibu kuhusu hatima yake Man United UKURASA 21



Wachezaji wa timu ya Taifa (Taifa Stars) wakiwa kwenye mazoezi katika Uwanja wa JMK Park kujiandaa na mchezo wa marudiano wa kufuzu michuano ya CHAN dhidi ya Somalia utakaochezwa leo, uwanja wa Benjamin Mkapa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Stars karata muhimu leo

## ●●● Inaivaa Somalia ikihitaji ushindi au sare ili kusonga mbele kwenye kufuzu CHAN...

**Shufaa Lyimo na Adam Fungamwango**

HATMA ya timu ya taifa ya Tanzania, Taifa Stars, kwenda kwenye hatua inayofuata kwa ajili ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa wachezaji wanaocheza ligi za nyumbani (CHAN), itafahamika leo itakaporudiana na Somalia kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Stars inaingia uwanjani ikiwa na mtaji wa bao moja ililolipata Jumamosi iliyopita kwenye uwanja huo huo, ilipoinyuka timu ya taifa ya Somalia bao 1-0 lililofungwa na Abdul Selemani "Sopu' dakika moja baada ya mapumziko.**

Wakati Stars ikihitaji ushindi au sare ya aina yoyote ili kuweza kusonga mbele, wageni Somalia wanahitaji ushindi wa zaidi ya bao moja ili kuweza kupita kwenye raundi inayofuata.

Timu yoyote itakayosonga mbele itakutaka na timu ya taifa ya Uganda, The Uganda Cranes.

Jumamosi iliyopita, timu hizo zilicheza kwenye uwanja huo huo, lakini kikanuni Somalia ilihesabika kuwa ipo nyumbani, baada ya wao wenyewe kuomba hivyo, kutokana na usalama mdogo kwenye nchi yao.

Kocha Mkuu wa timu hiyo Kim Poulsen amesema kuwa anatumaini mchezo wa leo utakuwa mzuri, tofauti na mechi iliyopita huku akiweka wazi kuwa watamkosa golikipa, Aishi Manula.

"Wachezaji wote wako sawa, isipokuwa Aishi ambaye aliumia kwenye mechi iliyopita, tumejiandaa kucheza kwa kushambulia zaidi na hapo hapo kujilinda ili tusiruhusu bao, falsafa yetu ni kupigiana pasi zaidi na kushambulia," alisema kocha huyo.

Aidha Poulsen alisema wachezaji wake wapo tayari kwa mchezo huo na anauchukulia kwa umuhimu mkubwa.

Kwa upande wake Aishi Manula alisema wachezaji wamejipanga kupata matokeo mazuri tofauti na waliyoyapata kwenye mchezo uliopita.

"Tumejipanga kupata matokeo bora katika mchezo huo tumeshawasoma wapinzani wetu tunaomba watanzania waendelee kutuombea na kutupa sapoti," alisema Manula.

"Mechi iliyopita tulikuwa na matarajio makubwa, lakini haikuwa kama tulivyotarajia, lakini kwenye mechi hii tuna uhakika kwa sababu tayari tumeshawaona jinsi wanavyocheza, jinsi walivyoweza kujilinda vizuri na sisi leo kama alivyosema mwalimu, tunakwenda kushambulia zaidi," alisema.

## Nkane azitisha Simba, Azam

**Na Adam Fungamwango**

WINGA wa Yanga Denis Nkane amesema yeye na wachezaji wenzake wa timu hiyo wameambizana kuhakikisha wanachukua vikombe vyote kwa mara nyingine na si vitatu tena, bali hata vile ambavyo vitakavyoongezeka.

Maneno hayo ya ujasiri ni kama kuzitisha klabu za Simba na Yanga ambazo nazo msimu huu zimesajili wachezaji mahiri kwa malengo ya kutwaa mataji, ikiwemo Ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza akiwa kambini Kigamboni ambako kikosi cha Yanga kimeweka kambi, Nkane ambaye kwa sasa wachezaji wenzake wamemtungia jina jipya la utani 'Boy From Buza', amesema wao kama wachezaji wanaendelea vizuri na mazoezi ya fizikia na kuuchezea mpira, lengo ni kufanya vema msimu ujao kuwafurahisha wanachama na mashabiki wa Yanga

"Kambi inakwenda vizuri, tunafanya mazoezi yote ya kuweka mwili sawa na kuuchezea mpira. Msimu ujao naamini kama mchezaji nina deni kubwa kwenye michuano ya ndani na nje ya nchi.

Naamini hili litafanyika nikiwa na ushirikiano na wachezaji wenzangu, tumejipanga kuchukua tena mataji yote matatu, ni kitu kinachowezekana kabisa na kama vingine vitaongezeka navyo tutavichukua," alisema Nkane, mchezaji aliyesajiliwa kipindi cha dirisha dogo msimu uliopita, akitokea Biashara United ambayo msimu ulipomalizika ikashuka daraja.

Alisema kuwa amejifunza vitu kadhaa kutoka kwa wachezaji Stephane Aziz Ki na Gael Bigirimana, kwa sababu ni wachezaji wakubwa na wameshacheza michuano mbalimbali mikubwa kuliko yeye.

"Nimefurahi na najivunia kucheza nao kwa sababu ni wachezaji wakubwa na mimi najifunza vitu kadhaa kutoka kwao, naamini muda utaongea na wanachama na mashabiki wa Yanga watafurahi," alisema.

Kikosi cha Yanga kinaendelea na mazoezi, huku wachezaji wawili wakiwa bado hawajawasili, nao ni Yannick Bangala na Bernard Morrison aliyesajiliwa kutoka Simba.

Licha ya kujiandaa na msimu mpya wa mashindano, lakini Yanga kwa sasa inajiandaa na tamasha la Wiki ya Mwananchi, kilele chake kikitarajiwa kufanyika Agosti 6 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, itakapocheza mechi, huku taarifa za ndani zikidai kuwa huenda ikacheza dhidi ya Vipers FC ambao ni Mabingwa wa Uganda.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042